epaper.ippmedia.com
MIAKA 30 Nipashe Mwanga wa Jamii
www.ippmedia.com

# Nipashe

Jumatano Novemba 20, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581866
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII

The Guardian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710
LIKE & FOLLOW US

## UCHAGUZI WA MITAA

# Jino kwa jino


Dorothy Semu


John Mnyika

- **Makada** CCM, upinzani watawanyika nchi nzima kusaka kura, Nape, Lissu, Zitto wapewa jukumu...

*Endelea ukurasa 2*


Balozi Dk. Emanuel Nchimbi

**Masharti** mapya yawekwa utoaji leseni uchimbaji madini nchini
UKURASA WA 8

**Kigogo** wa TPA akana kuwapo kazini zabuni ilipopitishwa
UKURASA WA 8

**Russia** kujibu vikali makombora ya Marekani, timu Trump yampinga Rais Joe Biden
UKURASA WA 19

### MAAFA KARIAKOO

**Waokolewa siku ya nne, Rais Samia aongeza muda uokoaji; Diva, Niffer wakamatwa**
UKURASA 3

# Mbowe: Tofauti za kifikra ndani ya CHADEMA ni mtaji kisiasa

UKURASA 4


Mwenyekiti wa CHADEMA Taifa, Freeman Mbowe, akizungumza na waandishi wa habari Dar es Salaam jana kuhusu maandalizi ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa. **PICHA: MIRAJI MSALA**



Skani hapa kutembelea chaneli yetu

**MICHEZO** **MSUVA AIPELEKA STARS AFCON 2025** UK.24

**MAONI,** UK.6




Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda (wa pili kushoto), akibonyeza kitufe kuzindua vitabu vitatu vilivyoshinda Tuzo ya Taifa ya Mwalimu Nyerere ya Uandishi Bunifu, jijini Dar es Salaam jana. Wengine ni Mwenyekiti wa Kamati ya tuzo hiyo, Prof. Penina Mlama (wa tatu kulia) na (wa pili kulia) ni Mkurugenzi wa Taasisi ya Elimu Tanzania (TET), Dk. Aneth Komba. **PICHA: MAULID MMBAGA**

# CCM, upinzani jino kwa jino Uchaguzi wa Mitaa

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

KAMPENI za Uchaguzi wa Serikali za Mitaa zinaanza leo hadi Novemba 26 mwaka huu: Chama Cha Mapinduzi (CCM), kimewagawa makada wake waandamizi kufanya uzinduzi wa kampeni za chama hicho mikoa yote nchini.

Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) nacho kimetangaza kuwa viongozi wakuu wa chama watashiriki kampeni za uchaguzi huo, wakigawanyika katika kanda nane za kichama.

ACT - Wazalendo nao hawako mbali katika harakati hizo, wakitangaza kuwa viongozi wa kitaifa, wakiongozwa na Kiongozi wa Chama, Dorothy Semu, wanatarajiwa kushiriki kampeni hizo katika mikoa yote ya Tanzania Bara kuanzia leo.

**MIKAKATI CCM**

Mitandao ya kijamii ya CCM inaonesha vigogo wa chama hicho ambao mikoa iko katika mabano, ndio watanguruma leo wakati wa uzinduzi huo.

Mjumbe wa Kamati Kuu na Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango (Dodoma), Katibu Mkuu wa CCM, Dk. Emmanuel Nchimbi (Mwanza), Mjumbe wa Kamati Kuu na Makamu wa Rais wa Pili Zanzibar, Hemed Suleiman Abdullah (Tanga), Waziri Mkuu Kassim Majaliwa (Kigoma), Naibu Waziri Mkuu Dk. Doto Biteko (Mara).

Naibu Katibu Mkuu wa CCM Zanzibar, Dk. Mohamed Said Mohamed (Katavi), Katibu wa NEC, Siasa na Uhusiano wa Kimataifa, Rabia Abdalla Hamid (Kilimanjaro), Makamu Mwenyekiti wa UWT, Zainab Shomari (Lindi), Katibu wa NEC - Idara ya Organizesheni, Issa Haji Ussi Gavu (Geita), Katibu wa Siasa, Itikadi na Uenezi, Amos Makalla (Dar es Salaam).

Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wazazi Taifa, Fadhil Maganya (Simiyu), Katibu Mkuu wa Jumuiya hiyo, Ally Hapi (Kagera), Mwenyekiti wa Umoja wa Vijana, Mohamed Kawaida (Morogoro), Katibu Mkuu wa Umoja huo, Jokate Mwegelo (Pwani), Naibu Katibu Mkuu CCM Bara, John Mongella (Mbeya), Spika wa Bunge na Rais wa Umoja wa Mabunge Duniani (IPU), Dk. Tulia Ackson (Songwe), Spika wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar, Zuber Ali Maulidi (Singida), Mwenyekiti wa UWT Taifa, Mary Chatanda (Arusha).

Wajumbe wengine wa Kamati Kuu na NEC waliopewa jukumu hilo ni pamoja na Waziri Mkuu mstaafu Mizengo Pinda (Mtwara), Halima Mamuya (Njombe), Nasir Ally Juma (Tabora), Mohamed Aboud (Iringa), Hussein Bashe (Shinyanga), Livingstone Lusinde (Manyara), Nape Nnauye (Rukwa) na Salim Faraji Abri (Asasi) aliyepangwa mkoani Ruvuma.

**KANDA 8 CHADEMA**

Akizungumza na waandishi wa habari jana mkoani Dar es Salaam, Mwenyekiti wa CHADEMA Taifa, Freeman Mbowe, alisema viongozi wakuu watatawanyika katika kanda zote kusaka kura za wagombea wao.

Alisema Makamu Mwenyekiti wa CHADEMA, Tundu Lissu, anatarajiwa kuzindua kampeni za Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, Vijiji na Vitongoji leo wilayani Ikungi, mkoani Singida.

Mbowe alisema akishafungua kampeni Ikungi, Lissu atakwenda kuzindua Tarime, mkoani Mara kesho.

Alitoa maelezo hayo baada ya kuulizwa na waandishi wa habari kuhusu kauli ya Lissu aliyoitoa hivi karibuni kwamba chama hicho kinapaswa kujipanga upya kwa Uchaguzi Mkuu kwa kudai Katiba Mpya kwa kuwa uchaguzi wa mitaa mwaka huu ni kama umeshaisha kutokana na kuenguliwa idadi kubwa ya wagombea wao.

"Makamu Mwenyekiti wetu (Lissu) alisema uchaguzi umevurugwa, ni kweli umevurugwa na kila mtu anaona na kusema hivyo, kila mwenye akili timamu anajua uchaguzi umevurugwa. Makamu Mwenyekiti hajawahi kusema tujitoe katika uchaguzi, kwa sababu anajua tulikubaliana nini kwenye vikao.

"Ndiyo sababu kesho (leo) anazindua kampeni Ikungi na keshokutwa yuko Tarime anazindua kampeni. Hii taarifa kwamba alitoa kauli uchaguzi umevurugwa, wamesema maaskofu, masheikh, wanazuoni, wanasiasa na hata waandishi wa habari.

"Hakumaanisha tujitoe, alisema uchaguzi umevurugwa. Kwani nani anasema uchaguzi haujavurugwa? Na anazindua huko na wengine tutatawanyika kuzindua maeneo mengine," alisema.

Mbowe alisema viongozi wakuu wa chama hicho wamepangiwa kanda na maeneo tofauti na kila mmoja atatakiwa kufanya kampeni hizo.

Mbowe alisema hoja ya Lissu kutaka CHADEMA ijipange upya, ni sahihi kwa kuwa mwisho wa uchaguzi mmoja ni mwanzo wa maandalizi wa uchaguzi mwingine.

"Uchaguzi mmoja ukiisha unazaa mwingine. Mchakato mmoja ukiisha hukati tamaa, unajipanga upya. Ndicho anachomaanisha, sasa shida iko wapi?" alihoji.

Mbowe alisema chama hicho kiko imara na kwamba tofauti za mawazo miongoni mwa viongozi, haimaanishi mpasuko bali ni kuimarika kwa wanasiasa hao.

"Ukishakuwa na chama cha siasa kisichokuwa na minyukano, hicho ni chama mfu. Siasa ndivyo ilivyo. Mkiona kwenye siasa mnakubaliana kila kitu kwa asilimia 100, hiyo safari hamtoboi," alisema.

Kuhusu Ilani za Uchaguzi, Katibu Mkuu wa CHADEMA, John Mnyika, alisema kila eneo limetakiwa kuandaa ilani kulingana na mazingira na vipaumbele vya wananchi.

"Hata hivyo, ajenda ya hali ngumu ya maisha inayowakabili wananchi wote, hitaji la Katiba mpya, Tume Huru ya Uchaguzi na kero ya huduma mbovu za kijamii ni mambo ambayo tutayabeba kwa ujumla," alisema Mnyika.

**ACT-WAZALENDO**

Chama cha ACT - Wazalendo kimesema viongozi wa kitaifa, wakiongozwa na Kiongozi wa Chama, Dorothy, wanatarajiwa kushiriki kampeni za Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, Vijiji na Vitongoji katika Mikoa yote ya Tanzania Bara kuanzia leo.

Kwa mujibu wa taarifa kwa umma iliyotolewa na Msemaji-Uchaguzi wa Serikali za Mitaa wa ACT- Wazalendo, Rahma Mwita, wakati wa kampeni hizo, viongozi hao wa kitaifa watawanadi wagombea wa ACT - Wazalendo kwenye vijiji na mitaa mbalimbali nchini.

Kiongozi wa Chama Dorothy na Makamu Mwenyekiti Bara, Isihaka Mchinjita wataongoza kampeni za viongozi wa kitaifa katika mikoa ya kichama Mwambao, Lindi, Mtwara na Selous.

Kiongozi wa Chama mstaafu, Zitto Kabwe, Mwenyekiti wa Ngome ya Wanawake, Janeth Rithe na Mwenyekiti wa Ngome ya Vijana, Abdul Nondo wataongoza kampeni za viongozi wa kitaifa mikoa ya Tabora, Katavi, Rukwa na Tabora.

Taarifa hiyo ya ACT - Wazalendo ilieleza kuwa Makamu Mwenyekiti Zanzibar, Ismail Jussa na Mjumbe wa Kamati Kuu, Rehema Ally wataongoza kampeni katika mkoa wa Tanga.

Katibu Mkuu, Ado Shaibu na Katibu wa Ngome ya Wazee, Janeth Fusi wataongoza kampeni za kitaifa mikoa ya Ruvuma, Iringa, Njombe, Mbeya na Songwe.

Naibu Katibu Mkuu Bara, Ester Thomas, akiambatana na Naibu Katibu wa Haki za Binadamu, Mbarala Maharagande wataongoza kampeni za viongozi wa kitaifa mikoa ya Shinyanga, Simiyu, Mwanza, Mara, Kagera na Geita.

Mwenyekiti wa Chama mstaafu, Juma Duni Haji ataongoza kampeni za kitaifa mkoani Dar es Salaam. Jumla ya mikutano 28 itafanyika.

Mwishoni mwa wiki, Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Mohamed Mchengerwa, alisema kuwa kati nafasi 80,430 zinazogombewa CCM imeweka wagombea katika nafasi zote huku vyama vingine 18 vya siasa vikiweka wagombea katika nafasi 30,977 sawa na asilimia 38.51.

Alifafanua kuwa kwa nafasi ya mwenyekiti wa kijiji, wanaotakiwa ni 12,280, vyama 18 vya siasa viliweka wagombea katika nafasi 6,060 sawa na asilimia 49.35 ya nafasi hizo.

"Nafasi za mwenyekiti wa mtaa zinazogombewa ni 4,264, lakini vyama 18 vya siasa viliweka wagombea katika nafasi 3,281 sawa na asilimia 76.94 ya nafasi hizo.

"Nafasi za mwenyekiti wa kitongoji zinazogombewa ni 63,886 ambapo vyama 18 vya siasa viliweza kuweka wagombea katika nafasi 21,636 sawa na asilimia 33.87 ya nafasi hizo," alisema.

Waziri Mchengerwa alisema hali hiyo ni kabla ya malalamiko ya kuenguliwa kinyume cha taratibu, hivyo huenda idadi ya wagombea kutoka vyama 18 vya upinzani ikapungua baada ya uamuzi wa rufani za mapingamizi.

***Imeandikwa na Augusta Njoji, DODOMA Restuta James**

*Kwa maoni kuhusu habari hii: Piga/sms / WhatsApp : +255 677 020 701*
*Email: customerrelations@guardian.co.tz*

# Wawili zaidi waokolewa jengo lililoporomoka

**Na Waandishi Wetu**

WAKATI muda wa uokoaji katika jengo lililoporomoka eneo la Kariakoo, Dar es Salaam, Jumamosi iliyopita ukiongezwa, watu wawili zaidi wameokolewa wakiwa hai.

Watu hao wamepatikana, mmoja juzi ikiwa ni siku ya tatu na jana siku ya nne tangu jengo hilo la ghorofa nne lililoko kati ya mitaa ya Congo na Mchikichnii, kuporomoka na kusababisha vifo vya watu 16 na majeruhi 88 hadi sasa.

Jana, Rais Samia Suluhu Hassan alimweleza Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, kuongeza saa 24 za uokoaji katika jengo hilo, huku akiwaita waokoaji wakiwamo wananchi waliojitokeza katika shughuli hiyo ni mashujaa wa taifa.

Wakizungumza kwa njia ya simu, Rais Samia alimweleza Waziri Mkuu kwamba anatambua utaratibu wa uokoaji una muda maalum wa saa 72 mpaka kusitishwa.

"Binafsi nina matumaini kuwa Mwenyezi Mungu anaweza akatenda miujiza yake na kuwanusuru ndugu zetu wengine ambao bado wamenasa kwenye jengo hilo.

"Ninakupa maelekezo ya kutositisha uokoaji na kuongeza muda wa saa 24 zaidi ili kuwapambania ndugu zetu ambao tunaamini bado wako hai," alisema Rais Samia kupitia taarifa iliyotolewa jana na Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais, Ikulu, Sharifa Nyanga.

Aidha, Rais Samia alipongeza vikosi vyote na wananchi wanaopambana kuokoa maisha ya wenzao walionasa katika vifusi.

"Ninaomba ufikishe salamu zangu na uwaeleze kuwa ninatambua na nina wathamini sana. Wameonesha utu, uzalendo mkubwa na uchapakazi wa hali ya juu sana," alisema.

Rais Samia pia aliwatia moyo na kuwapa nguvu ya kuendelea kuwapambania wenzao na kuwaombea Mungu awalinde na kuwapa nguvu wakati wote wakitekeleza jukumu hilo kubwa la kizalendo.

Aliwasihi wananchi, ndugu na jamaa kuendelea kuwa na subira na kama taifa wanaendelee kuwaombea ili mchakato wa uokoaji ufanikiwe.



**WAWILI WAOKOLEWA**

Akizungumza na vyombo vya habari katika eneo la tukio, Msemaji Mkuu wa Serikali, Thobias Makoba, alisema juzi na jana waliokolewa watu wawili.

Alisema majeruhi wa kwanza aliokolewa juzi usiku baada ya hafla ya kuaga miili 15 kati ya 16 ya waliofariki dunia katika tukio hilo na wa pili aliokolewa jana mchana ma kwamba hadi sasa majeruhi wamefikia 88.

"Haiwezekani watu ambao hawako katika eneo la tukio kuelewa mchakato mzima kutokana na jengo lilivyoanguka. Huwezi kuondoa vifusi na greda. Ni muhimu kufanya kwa uangalifu ili kuzuia jengo kuporomoka zaidi," alisema Thobias.

Nipashe ilishuhudia wananchi ambao bado hawajaona ndugu zao wakiwa pembezoni mwa eneo hilo wakisubiri kuona hatima ya wapendwa wao waliofukiwa na kifusi cha jengo hilo.

**WACHANGISHAJI MBARONI**

Katika hatua nyingine, Jeshi la Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam, limewakamata na kuwahoji Diva Malinzi (36) mkazi wa Mikocheni na Jenifer Bilikwija (25) mkazi wa Salasala, Dar es Salaam kwa madai ya uchangishaji fedha za tukio hilo. Jeshi hilo limesema suala hilo ni kinyume cha sheria na kanuni zinazoshughulikia majanga.

Kamanda wa Polisi Kanda hiyo, Kamishna Msaidizi Mwandamizi (SACP) Jumanne Muliro, alisema watu hao wamekamatwa kwa kukusanya fedha kwa kutumia akaunti zao binafsi.

Alisema Bilikwija, maarufu kama Niffer, alikamatwa jijini Dodoma na kurejeshwa Dar es Salaam, huku Diva akikamatwa Dar es Salaam.

"Wakati jitihada mbalimbali zikifanywa na serikali na sekta binafsi kuhusiana na namna ya kuwaokoa watu, zilipatikana taarifa za watu wasio na mamlaka yoyote ya kisheria ya kushughulikia majanga yenye sura ya kitaifa, kuanza kukusanya fedha kwa kutumia akaunti zao binafsi suala ambalo ni kinyume cha sheria na kanuni zinazoshughulikia majanga.

"Jeshi la Polisi litashirikiana na mamlaka zingine za kisheria kuona hatua zaidi zinazopaswa kuchukuliwa dhidi ya watuhumiwa hao," alisema.

Kamanda Muliro alisema Jeshi la Polisi linaendelea kutoa tahadhari na halitasita kuchukua hatua za kisheria kwa mtu au watu ambao yanapotokea matatizo au majanga wanaona ni fursa kujinufaisha.

**Imeandaliwa na Romana Mallya, Halfan Chusi na Joyce Lameck**

*Kwa maoni kuhusu habari hii: Piga/sms / WhatsApp : +255 677 020 701*
*Email: customerrelations@guardian.co.tz*


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA FEDHA**

**MWALIKO WA KUSHIRIKI MKUTANO WA PILI WA JUMUIYA YA WAHASIBU WAKUU WA SERIKALI AFRIKA-AAAG**

Tanzania inatarajia kuwa mwenyeji wa Mkutano Mkuu wa Wahasibu wa Serikali wa Afrika mwaka 2024 (AAAG) utakaofanyika jijini Arusha kuanzia tarehe 2 hadi 5 Desemba, 2024.

Mkutano wa pili wa Jumuiya ya Wahasibu Wakuu wa Serikali Afrika utakuwa na mada mtambuka ambazo zitasaidia watumishi wa kada mbalimbali kuwaongezea ujuzi na Maarifa.

Pia Mkutano huu utasaidia Viongozi na Watumishi wa Tanzania kupata nafasi ya kubadilishana uzoefu na kupeana fursa na Viongozi na Watumishi toka nchi nyingine za Afrika, Benki ya Dunia na IMF. Mgeni rasmi anatarajiwa kuwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Ada ya ushiriki ya mkutano ni **Shilingi za Kitanzania 1,300,000/=** kwa kila mshiriki. Hivyo, Mamlaka husika zinaombwa kuwaruhusu na kuwalipia Wahasibu, Wakaguzi wa Ndani, Maafisa Usimamizi wa Fedha, Maafisa TEHAMA na watumishi wa kada nyingine kuhudhuria mkutano huu.

Washiriki wote wanatakiwa kuanza kijisajili kupitia lango (portal) lifuatalo: https://conference.aaag.org.zm kuanzia sasa hadi tarehe 01 Disemba, 2024 na ada ya ushiriki ilipwe kupitia **akaunti namba 9924915301 yenye jina African Association of Accountants General (AAAG).**

Aidha, kwa Taasisi za Umma, Kampuni mbalimbali na watu binafsi wanaotaka kudhamini Mkutano huu kwa lengo la kujitangaza kibiashara na kufanikisha Mkutano huu; Wizara ya Fedha inawakaribisha.

Kwa mawasiliano zaidi piga Namba ya simu +255 713 525 592 barua pepe, veronica.kishala@hazina.go.tz na evans.sayile@hazina.go.tz Sanduku la Posta ni Katibu Mkuu, Wizara ya Fedha S.L.P 2802, Dodoma.

Pia kama muombaji amesahau namba ya simu, barua pepe na Sanduku la Posta anaweza kupata mawasiliano kupitia wakuu wa Hazina Ndogo waliopo kila mkoa Tanzania bara na Ofisi ya Mhasibu Mkuu wa Serikali Zanzibar.

**Kwa Nakala Ngumu tafadhali wasilisha kwa anuani ifuatayo:**

**Sekretariati ya Kamati ya Maandalizi Mkutano wa AAAG,**
**Wizara ya Fedha**
**Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali**
**Jengo la Hazina (Ghorofa ya Pili),**
**18 Barabara ya Jakaya Kikwete,**
**S.L.P 2802,**
**DODOMA.**

**Tangazo hili limetolewa na:**

**KATIBU MKUU - HAZINA**
**Novemba, 2024**

HABARI KITAIFA

# Mbowe: Tofauti kifikra ndani ya CHADEMA ni mtaji kisiasa

**Na Restuta James**

MWENYEKITI wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) Taifa, Freeman Mbowe, amesema chama hicho kiko imara, akisisitiza kwamba tofauti za mawazo miongoni mwa viongozi, hazina maana kuwapo mpasuko bali ni kuimarika kwa wanasiasa hao.

Mbowe aliyasema hayo jana mkoani Dar es Salaam alipozungumza na waandishi wa habari kuhusu msimamo wa chama hicho dhidi ya kinachoendelea katika mchakato wa Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, Vijiji na Vitongoji uliopangwa kufanyika tarehe 27 mwezi huu.

Alitoa ufafanuzi wa kile kinachoonekana ni mnyukano ndani ya CHADEMA, baada ya Makamu Mwenyekiti wake, Tundu Lissu kudai kuwa chama hicho kinapaswa kujipanga upya kwa Uchaguzi Mkuu mwakani kwa kuwa wa sasa umeshakwisha kutokana na kuenguliwa kwa idadi kubwa ya wagombea wake katika mitaa, vijiji na vitongoji.

Pia kauli ya Mwenyekiti wa Kanda ya Kaskazini, Godbless Lema, kumtuhumu Naibu Katibu Mkuu wa CHADEMA Bara, Benson Kigaila, kwamba amehusika na vurugu zilizotokea wakati wa uchaguzi wa viongozi wa chama hicho mkoani Arusha.

"Hatuna ugomvi, hayo ni mambo ya kawaida tu. Ukishakuwa na chama cha siasa kisichokuwa na minyukano, hicho chama ni mfu. Siasa ndivyo ilivyo. Mkiwa kwenye siasa mnakubaliana kila kitu kwa asilimia 100 siku zote, hiyo safari hamtoboi.

"Kuna wakati viongozi wanateleza, lakini kusema eti tuna mnyukano ambao utaua chama hiki, sikilizeni, hiki chama kina miaka 30 na kimefika hapa kwa maumivu makubwa yetu sote.

"Sisi sote tumeshaapa tutakilinda kwa gharama yoyote ile. Kama kuna mtu anafikiria kwamba kuna mgogoro CHADEMA ambao utakigawa chama, niwaambie sisi ni wamoja. Watu watanyukana lakini sisi ni wamoja.

"Hiki chama si cha Mbowe, wala Lissu, wala Mnyika; ni cha watanzania wengi, ambao ni wana CHADEMA na wengine wala siyo wana CHADEMA, lakini wana maslahi na chama hiki kwa sababu kina maslahi ya taifa," Mbowe alisema kwa hisia kali.

Alisema viongozi wakuu hadi wa ngazi ya chini, wanawajibika kukilinda kwa lengo la kujenga demokrasia nchini, lakini akatoa angalizo kuwa kwenye minyukano hiyo, viongozi wanapokosea, wanawarekebisha ndani ya vikao.

Mwenyekiti huyo alisema kauli ya Lissu kuhusu uchaguzi, imetafsiriwa vibaya kwa kuwa hakumaanisha CHADEMA ijiondoe, bali kijipange kwa ajili ya uchaguzi ujao.

**KUENGULIWA WAGOMBEA**

Mbowe alisema msimamo wa CHADEMA ni kushiriki uchaguzi, hata kama atabakia mgombea mmoja kwenye ujumbe au uenyekiti na kuonya kwamba wagombea waliobakishwa, wasiingie katika mtego wa kujiondoa.

Alisema wanashiriki uchaguzi ambao mchakato wake umevurugwa katika hatua mbalimbali, kuanzia utungaji sheria na kanuni, uandikishaji, wasimamizi, uchukuaji fomu na urejeshaji, kuenguliwa kwa wagombea na kukata rufani.

Mbowe alisema msimamo wa kuendelea kushiriki uchaguzi, ulitolewa na kikao cha Kamati Kuu iliyokutana mkoani Mtwara Machi mwaka huu, hivyo hawawezi kukiuka maelekezo hayo.

Alisema ukiukaji wa sheria, kanuni na taratibu za uchaguzi, umefanywa kwa makusudi, akidai kuwa ni marudio ya kilichofanywa katika uchaguzi wa mwaka 2019 na 2020 licha ya ahadi za viongozi wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) na serikali, kwamba makosa hayo hayatajirudia.

"Mwaka 2019, tulijitoa, safari hii hatujitoi na tunataka tuende nao hivi hivi hadi hatua ya mwisho. Tunasema watu wetu wapambane mpaka tone la mwisho," alisema.

Mbowe alisema kuwa mwaka 2015, CHADEMA ilikuwa na wabunge 72, madiwani 1,104, wenyeviti wa mitaa 980 sawa na asilimia 25.4 ya mitaa yote, jambo lililoiwezesha kuongoza majiji ya Dar es Salaam, Arusha, Mbeya, Mwanza na Halmashauri za Shinyanga, Moshi na Bukoba.

Alisema CHADEMA kilikuwa na wenyeviti wa vijiji 1,754, wenyeviti wa vitongoji 9,145, wajumbe mchanganyiko 18,527 na wajumbe wanawake 10,471.

Alisema hadi jana, wagombea wa CHADEMA ambao walibakia kugombea nafasi uenyekiti wa mitaa ni 2,886, vijiji ni 4,175 na vitongoji ni 14,805.

"Jumla tuna wagombea wastani wa vitongoji, mitaa na vijiji asilimia 33.2. Pamoja na kwamba si kazi nyepesi kuwapata hao, wanachama wetu wameweza kuijenga demokrasia," alisema.

Alisema kwenye wajumbe mchanganyiko, nafasi zinazogombewa ni 252,154 na wagombea wa CHADEMA waliobakishwa ni 90,991 sawa na asilimia 36.

Mbowe pia aliwashukuru viongozi wa dini na wanaharakati kwa kusimama kutetea taifa, wakiwamo maaskofu na mashekhe.

Awali, Katibu Mkuu wa CHADEMA, John Mnyika, alisema kauli ya Waziri wa Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Mohamed Mchengerwa, kwamba vyama vyote vya siasa vilikubali kanuni na sheria za uchaguzi, si ya kweli kwa kuwa chama hicho kilipeleka mapendekezo na kupinga kile walichoona hakifai katika kila hatua.

*Kwa maoni: +255 677 020 701*
*Email: customerrelations@guardian.co.tz*




Mwanasaikolojia kutoka Taasisi ya Tanzania Health and Medical Education (TAHMEF), Catherine Kisarika (kulia), akifafanua jambo kuhusu uwiano binafsi na maisha ya kazi, wakati wa mafunzo ya afya ya akili kwa wafanyakazi wa Kampuni ya IPP Media, katika Chumba cha Habari cha kampuni ya The Guardian Ltd (TGL) inayochapisha magazeti ya The Guardian na Nipashe, Mikocheni, Dar es Salaam jana. **PICHA: JOHN BADI**

# TAHMEF yatoa mafunzo ya afya akili kwa wafanyakazi The Guardian

**Na Grace Mwakalinga**

WAANDISHI wa habari wametakiwa kufanya uwiano wa maisha yao binafsi na kazi ili kuboresha ustawi wao wa kimwili na kiakili kuepuka magonjwa yasiyoambukiza ukiwamo wa afya ya akili.

Akitoa mafunzo kwa wafanyakazi wa Kampuni ya The Guardian Limited jana, Mwanasaikolojia kutoka Tanzania Health and Medical Education Foundation (TAHMEF), Paul Ndemanisho, alisisitiza umuhimu wa wafanyakazi kutathmini vipaumbele vyao na kujitahidi kudumisha uwiano mzuri kati ya kazi na maisha binafsi.

Alisema ni muhimu kupanga ratiba inayowapa nafasi ya kupumzika, kuwekeza muda kwenye familia, na kujitathmini ili kupunguza athari za uchovu wa mwili na msongo wa mawazo unaosababishwa na changamoto za kazi.

TAHMEF inatoa mafunzo na huduma ya kisaikolojia kupitia wataalamu wake wenye leseni ya kutoa ushauri kwa mtu mmoja mmoja na vikundi kupitia video, kupiga simu na mafunzo ya ana kwa ana.

Ndemanisho alisema, ingawa uandishi wa habari ni kazi yenye mchango mkubwa kwa jamii, ni muhimu wakatoa kipaumbele kwa afya zao, kwa kuwa ustawi wao binafsi ni muhimu kwa kuboresha utendaji kazi wao.

"Waandishi wa habari wanahitaji kutafuta muda wa kupumzika na kuwekeza katika familia zao, hii sio tu itaboresha ustawi wa maisha yake binafsi, bali pia itasaidia kuboresha utendaji kazi wake, kuwa na uwiano na maisha binafsi ili kuondoa athari za uchovu na msongo wa mawazo," alisema Ndemarisho.

Mhariri Mtendaji wa gazeti The Guardian, Wallace Maugo, alisisitiza kuwa mafunzo hayo ni muhimu kwa waandishi wa habari, kwa kuwa yanawasaidia kuelewa ustawi mzuri wa kimwili na kiakili.

Aliwashauri viongozi wa vyombo vya habari kujengewa uwezo ili waweze kusaidia wafanyakazi wao kutengeneza ratiba inayowezesha kufanya kazi kwa ufanisi huku pia wakidumisha uwiano na maisha yao binafsi.

"Majukumu ya waandishi ni makubwa na mara nyingi yanawafanya kushindwa kujumuika na jamii zao, lakini hii si kwa sababu hawataki, ni muhimu kwa viongozi kujua jinsi ya kuwasaidia waandishi kuwa na muda wa kupumzika na kushirikiana na familia zao," alisema Maugo.

> **"Waandishi wa habari wanahitaji kutafuta muda wa kupumzika na kuwekeza katika familia zao, hii sio tu itaboresha ustawi wa maisha yake binafsi, bali pia itasaidia kuboresha utendaji kazi wake, kuwa na uwiano na maisha binafsi ili kuondoa athari za uchovu na msongo wa mawazo."**

Mwanasaikolojia Catherine Kisarika, alisema changamoto za kifedha zimekuwa chanzo kikubwa cha matatizo ya afya ya akili kwa waandishi wa habari.

Alihimiza matumizi ya teknolojia ya huduma za afya ya akili zinazoweza kuwasaidia waandishi na watu wengine kuboresha ustawi wao wa kiakili, hasa kwa wale wanaokutana na changamoto za kifedha na za kijamii.

"Programu tumizi (Application) zinazotoa huduma za afya ya akili zinajitahidi kufikia watu wengi, na zinasaidia kutoa majibu ya haraka kuhusu matatizo ya kiakili.

Alisema ni muhimu kwa waandishi wa habari, kwa kuwa wengi wao wanakutana na msongo wa mawazo unaotokana na kazi zao," alisema Kisarika.

Mafunzo ya afya ya akili yanatoa fursa ya kujifunza namna ya kudumisha ustawi mzuri katika mazingira ya kazi yanayowabana.

## HABARI KITAIFA

# Anayeshtakiwa kuua mke wake kwa magunia ya mkaa ana kesi ya kujibu

**Na Grace Gurisha**

MFANYABIASHARA Khamis Luwongo (38) anayeshtakiwa kwa kumuua mkewe Naomi Marijani kisha kuuchoma moto mwili wake kwa kutumia magunia mawili ya mkaa, amepatikana na kesi ya kujibu, baada ya Mahakama kusikiliza mashahidi 14 wa upande wa mashtaka.

Aidha, wakili wa mshtakiwa, Hilda Mushi, aliiomba Mahakama Kuu Kanda ya Dar es Salaam imruhusu mteja wake atumie ripoti iliyotoka Hospitali ya Taifa ya Afya ya Akili Mirembe iliyoonesha kwamba wakati akitenda kitendo hicho, hakuwa timamu.

Jaji Hamidu Mwanga alitoa uamuzi huo juzi baada kupitia ushahidi uliotolewa na pamoja na vielelezo na kuona mshtakiwa ana kesi ya kujibu na atatakiwa kujitetea. Baada ya kuelezwa ana kesi ya kujibu, mshtakiwa alidai atajitetea kwa kiapo.

Mahakama pia ilipokea vielelezo mbalimbali katika kesi hiyo kama nyaraka ya maelezo ya onyo, maelezo ya ungamo, simu, laini za simu na udongo wenye masalia ya mafuta yanayodhaniwa kuwa ni ya Naomi.

Licha ya kuomba kutumia taarifa ya afya, mbele ya Jaji Elizabeth Mkwizu, mshtakiwa alikataa kwenda kupimwa akili na kudai kwamba yeye ni mzima wa afya na hana tatizo la akili, hivyo kwenda Mirembe ni kupoteza muda.

Pia akiwa mbele ya Jaji Mwanga, alidai kwamba aliyekuwa wakili wake, Mohamed Majaliwa, alishindwa kumzuia kwenda kupimwa akili Mirembe kwa madai kuwa yuko timamu.

Jaji Mwanga alikubaliana na ombi hilo la mshtakiwa kutumia ripoti hiyo katika utetezi wake ambayo iko kwenye mwenendo wa kesi hiyo.

Wakati Shahidi wa 13, Koplo Samwel, anatoa ushahidi wake akiongozwa na Wakili wa Serikali Mkuu, Yasinta Peter, alidai kuwa mwaka 2019 alikuwa akifanya kazi Kituo cha Polisi Kigamboni.

Alidai kuwa Julai 16, 2019 saa 8:00 mchana, akiwa kazini alielekezwa na Mkuu wa Upelelezi, Malelo kuongoza na timu ya upelelezi kwenda Gezaulole kwenye nyumba ya Khamis au Meshack ili kufanya upelelezi, akiwaongoza na mshtakiwa mwenyewe.

Alidai mshtakiwa Khamis aliwaonesha sehemu marehemu alikodondokea na kulikuwa na damu chini na kitandani na wataalamu wa Kitengo cha Uchunguzi wa Kisayansi waliendelea na kazi yao.

Pia aliwaongoza alikotoa nje mwili wa marehemu kwenye banda la kuku ambalo alitengeneza shimo akaujaza mkaa akauchoma na akawaonesha sehemu ambayo alimchomea moto.

Alidai kuwa kwenye banda hilo kulikuwa na damu ambayo mshtakiwa alidai ni zake ambazo alijiumiza wakati akitoa masalia ya marehemu ambayo aliyatia kwenye mfuko wa saruji na kuyapeleka kijiji cha Marogoro, Mkuranga mkoani Pwani.

"Nilichora ramani ya tukio mahali mauaji yalifanyika na mwili ulikochomewa. Kisha mshtakiwa aliwaongoza katika Kijiji cha Marogoro Kata ya Vikindu Wiliaya ya Mkuranga," alidai.

Koplo Samwel alidai walipofika eneo hilo kiongozi wa msafara aliwaita majirani pamoja na viongozi wa kijiji na mshtakiwa aliwapeleka sehemu alikozika masali ya mwili wa marehemu ambako wakikuta mashina matatu ya migomba.

Alidai kuwa mshtakiwa aliwaeleza kuwa mabaki ya mwili wa marehemu aliyazikia kwenye mgomba wa kwanza,walifukua kwenye wakakuta masalia majivu na mafuta na mifupa na meno yaliyoungua.

"Timu ya 'forensic' iliendelea na kazi yao yeye alichora ramani ya eneo la tukio akiongozwa na mshtakiwa Luwongo. Wakati anatuongoza alikuwa kwenye hali nzuri na ndio maana tulipofikia shambani alituonesha kuwa masalia ya marehemu aliyazima kwanya mgomba huu," alidai.

Alidai kuwa walifika shambani jioni saa 12:30 jua likiwa limeshazama, hivyo walitumia mwanga wa tochi na taa za magari waliyokuwa nayo. Luwongo alitia saini ramani hizo zote, kazi hiyo ilimalizika saa 4:00 usiku.

Pia shahidi wa 14, Koplo Mkombozi, ambaye ni mstaafu wa Jeshi la Polisi akiongonzwa na Wakili wa Serikali Mwandamizi, Ashura Mnzava, alidai kuwa mwaka 2019 alikuwa anafanya kazi Idara ya Upelelezi wa Makosa ya Jinai. Ofisi ya ZCO (Mkuu wa Upelelezi wa makosa ya Jinai Kanda Maalum ya Dar es Salaam)

Alidai kuwa alielekezwa na kiongozi wake akaandae timu ya ukaguzi wa matukio na mtuhumiwa aliwaongoza kuwapeleka eneo la tukio.




Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Reli Tanzania (TRC), Masanja Kadogosa, akikata utepe wakati wa ufunguzi wa duka la Airtel katika kituo cha SGR Dar es Salaam. Kushoto ni Mkurugenzi Mtendaji wa Airtel Tanzania, Charles Kamoto, Mwenyekiti wa Bodi ya Airtel Tanzania, Eliud Sanga na Mkurugenzi wa Huduma kwa Wateja, Adrianna Lyamba.


airtel money

TUMA NA KUTOA PESA BILA TOZO

ADA ZA MIAMALA YA AIRTEL MONEY

TOA PESA KWA WAKALA/ATM

| Kutoka (TSH) | Kwenda (TSH) | Ada ya Airtel Money | Tozo ya Serikali | Jumla makato | Unalipa bila Tozo |
|---|---|---|---|---|---|
| 100 | 999 | 190 | 10 | 200 | 200 |
| 1,000 | 1,999 | 310 | 10 | 320 | 320 |
| 2,000 | 2,999 | 390 | 10 | 400 | 400 |
| 3,000 | 3,999 | 590 | 14 | 604 | 604 |
| 4,000 | 4,999 | 640 | 27 | 667 | 667 |
| 5,000 | 6,999 | 950 | 54 | 1,004 | 1,004 |
| 7,000 | 9,999 | 1,000 | 56 | 1,056 | 1,056 |
| 10,000 | 14,999 | 1,450 | 102 | 1,552 | 1,552 |
| 15,000 | 19,999 | 1,450 | 195 | 1,645 | 1,645 |
| 20,000 | 29,999 | 1,850 | 306 | 2,156 | 2,156 |
| 30,000 | 39,999 | 1,850 | 351 | 2,201 | 2,201 |
| 40,000 | 49,999 | 2,300 | 419 | 2,719 | 2,719 |
| 50,000 | 99,999 | 2,600 | 573 | 3,173 | 3,173 |
| 100,000 | 199,999 | 3,500 | 707 | 4,207 | 4,207 |
| 200,000 | 299,999 | 5,100 | 821 | 5,921 | 5,921 |
| 300,000 | 399,999 | 6,200 | 838 | 7,038 | 7,038 |
| 400,000 | 499,999 | 6,700 | 982 | 7,682 | 7,682 |
| 500,000 | 599,999 | 7,200 | 1,245 | 8,445 | 8,445 |
| 600,000 | 699,999 | 7,600 | 1,532 | 9,132 | 9,132 |
| 700,000 | 799,999 | 7,600 | 1,700 | 9,300 | 9,300 |
| 800,000 | 899,999 | 7,600 | 1,750 | 9,350 | 9,350 |
| 900,000 | 1,000,000 | 7,600 | 1,776 | 9,376 | 9,376 |
| 1,000,001 | 3,000,000 | 7,600 | 1,875 | 9,475 | 9,475 |
| 3,000,001 | 5,000,000 | 9,500 | 2,000 | 11,500 | 11,500 |

| TUMA PESA AIRTEL - AIRTEL: Ada ya Airtel Money | Tozo ya Serikali | Jumla makato | TUMA PESA MITANDAO MINGINE: Ada ya Airtel Money | Tozo ya Serikali | Jumla Makato | LIPA KWA AIRTEL MONEY: Ada ya Airtel Money | Tozo ya Serikali | Jumla Makato | TUMA PESA KWENDA BANK: Ada ya Airtel Money | Tozo ya Serikali | Jumla Makato |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 10 | - | 10 | 10 | - | 10 | 20 | - | 20 | 140 | - | 140 |
| 25 | - | 25 | 45 | - | 45 | 50 | - | 50 | 220 | - | 220 |
| 25 | - | 25 | 45 | - | 45 | 70 | - | 70 | 400 | - | 400 |
| 40 | - | 40 | 90 | - | 90 | 100 | - | 100 | 450 | - | 450 |
| 50 | - | 50 | 90 | - | 90 | 200 | - | 200 | 600 | - | 600 |
| 120 | - | 120 | 180 | - | 180 | 300 | - | 300 | 710 | - | 710 |
| 140 | - | 140 | 180 | - | 180 | 500 | - | 500 | 1,000 | - | 1,000 |
| 325 | - | 325 | 495 | - | 495 | 500 | - | 500 | 1,250 | - | 1,250 |
| 350 | - | 350 | 495 | - | 495 | 850 | - | 850 | 1,430 | - | 1,430 |
| 360 | - | 360 | 540 | - | 540 | 920 | - | 920 | 1,430 | - | 1,430 |
| 375 | - | 375 | 612 | - | 612 | 1,000 | - | 1,000 | 1,930 | - | 1,930 |
| 380 | - | 380 | 675 | - | 675 | 1,200 | - | 1,200 | 2,120 | - | 2,120 |
| 675 | - | 675 | 1,125 | - | 1,125 | 1,700 | - | 1,700 | 2,780 | - | 2,780 |
| 940 | - | 940 | 1,440 | - | 1,440 | 2,000 | - | 2,000 | 3,740 | - | 3,740 |
| 1,200 | - | 1,200 | 1,710 | - | 1,710 | 2,600 | - | 2,600 | 4,600 | - | 4,600 |
| 1,450 | - | 1,450 | 2,070 | - | 2,070 | 3,000 | - | 3,000 | 4,700 | - | 4,700 |
| 1,450 | - | 1,450 | 2,250 | - | 2,250 | 3,300 | - | 3,300 | 5,200 | - | 5,200 |
| 2,100 | - | 2,100 | 2,880 | - | 2,880 | 4,500 | - | 4,500 | 5,400 | - | 5,400 |
| 3,100 | - | 3,100 | 3,870 | - | 3,870 | 5,500 | - | 5,500 | 5,400 | - | 5,400 |
| 3,100 | - | 3,100 | 3,870 | - | 3,870 | 5,700 | - | 5,700 | 5,500 | - | 5,500 |
| 3,250 | - | 3,250 | 3,870 | - | 3,870 | 6,000 | - | 6,000 | 5,500 | - | 5,500 |
| 3,300 | - | 3,300 | 5,400 | - | 5,400 | 6,000 | - | 6,000 | 5,500 | - | 5,500 |
| 4,000 | - | 4,000 | 5,400 | - | 5,400 | 6,000 | - | 6,000 | 7,500 | - | 7,500 |
| 4,000 | - | 4,000 | 5,400 | - | 5,400 | 6,000 | - | 6,000 | 9,000 | - | 9,000 |

BILA TOZO

FANYA MALIPO KWA AIRTEL MONEY

GePG MALIPO YA SERIKALI · LUKU · VING'AMUZI · MAJI · POLISI · SOLAR · BIDHAA MITANDAONI · MIAMALA YA KIBENKI · TRA · BRELLA · ARDHI · NDEGE · BIMA · VIKOBA · LIPA MITANDAO YOTE

Fanya yote na My Airtel App!
Pakua katika simu yako.

Download on the App Store · ANDROID APP ON Google play

Fanya malipo ya Serikali na bili mbalimbali kupitia My Airtel App

SUMATRA · Wizara ya Nishati na Madini · BRELA · Wizara ya Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi · dawasco

KUMBUKA

- Unaweza kuweka ama kupokea hadi Tsh 10,000,000 kwa siku na unaweza kutoa ama kutuma hadi Tsh 5,000,000 kwa siku kama usajili wako umekamilika na Airtel Money.
- Kila mara unapotuma pesa, kumbuka kuhakiki namba ya mpokeaji kuepuka kukosea na usumbufu.
- Airtel Money huonesha salio kwenye kila muamala. Endapo utafanya muamala wa kuangalia salio, kuangalia miamala miwili ya mwisho, taarifa ya muamala, muhtasari wa siku iliyopita, muhtasari wa siku, miamala ya mwezi uliopita, utatozwa gharama ya Tsh 50 kwa kila muamala.
- Kuwasiliana na Huduma kwa Wateja, Piga 100 bure au tembelea duka lolote la Airtel Money Branch.

Novemba, 2024

HARAKA.SALAMA.BILA MIPAKA.

## MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Kila mtu anahitaji kujua umuhimu wa afya ya akili

**AFYA** ya akili ni sehemu muhimu ya mwili wetu, ni lazima kutunza afya yetu ya kimwili ili kuepuka magonjwa makubwa yakiwamo yasiyo ya kuambukiza.

Kwa mujibu wa watalaamu wa afya, kila mtu ana tatizo la afya ya akili na hii hujidhihirisha jinsi watu wanavyochukua uamuzi kwa sababu yanafanyika kutokana na kile kilicho akilini.

Wataalam wanaeleza kuwa, afya ya akili huleta madhara mtu anapoamua kuzingatia "tatizo ni nini" badala ya "kile kilicho kizuri na kinachoendelea vizuri". Wengi wanaweza kujua dalili za magonjwa ya kimwili, kama vile mshtuko wa moyo au kiharusi, lakini hawajui afya mbaya ya akili.

Kwanini afya ya akili ni muhimu ni kwa sababu inaathiri mawazo, tabia na hisia. Kuwa na afya njema kihisia na kiakili kunaweza kukuza tija na ufanisi katika shughuli za kila siku za maisha. Pia ina jukumu muhimu kudumisha miunganisho ya kijamii, uhusiano, na inaruhusu mtu kuzoea mabadiliko katika maisha na kukabiliana na shida.

Ndio maana kuna kila sababu ya watu kufahamu afya ya akili ili waweze kufanyakazi kwa tija.

Mambo madogo au hatua zinaweza kusaidia katika kuimarisha afya ya akili. Wataalam wa afya wameelekeza njia chache za kukabiliana na tatizo mahususi la afya ya akili, kushughulikia hisia kali vizuri zaidi, au tu kujisikia chanya na mwenye nguvu zaidi.

Mambo yanayoshauriwa na wataalam hao ni kufanya uhusiano wa kijamii kuwa kipaumbele, kulenga kwa dakika 30 za shughuli kila siku, kula chakula cha ubongo chenye uwiano na afya, kufanya wakati wa burudani kuwa kipaumbele, kukumbuka, kushukuru, kulala

kwa saa saba hadi tisa za usingizi bora kila usiku, kutenga muda wa kutafakari (kutathmini upya) na kuthamini bila kupita kiasi.

Afya ya akili inaweza kuathiri watu tofauti kwa njia tofauti. Ikiwa juhudi zote za mara kwa mara za kuboresha afya hiyo na kihisia bado haisaidii ufanye kazi ipasavyo nyumbani, kazini au katika mahusiano yako, unaweza kuwa wakati wa kutafuta usaidizi wa kitaalamu.

Mtu anapoanza kuona mabadiliko katika furaha na mahusiano yao kwa ujumla, daima kuna njia chanya za kupata chakula kinachohitajika.

Baadhi ya njia za kupata usaidizi ni kuunganishwa na marafiki na familia, ambayo inapendekezwa kufikia watu maishani ambao wanaweza kusaidia kutoa msaada wa kihemko.

Kujifunza juu ya afya ya akili, hapa inaelezwa kuwa kuna nyenzo nyingi ambazo mtu anaweza kugeukia kwa kujifunza zaidi kuhusu afya ya kihisia.

Aidha, kutafuta msaada wa kitaalamu, hasa kwa mwanasaikolojia au mtaalamu wa magonjwa ya akili na kupata usaidizi wa kibinafsi mtu anaoutaka.

Afya ya akili inaweza kuathiriwa na mambo mbalimbali, ikiwa ni pamoja na matukio ya maisha au hata maumbile yako. Hatimaye, afya ya akili ni hali ya ustawi na si tu kutokuwapo au kuwapo kwa hali ya afya ya akili.

Wataalam wanaeleza kuwa mtu anapokuwa na hasira nyingi, sio dalili nzuri hivyo inampasa kwenda kumuona mwanasaikolojia ili aweze kumsaidia kwa sababu ni moja ya dalili ya kuwa na tatizo katika afya ya akili.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:

**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita, 0713 578 284
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge

Na Moshi Lusonzo

# Ajabu kuchangamkia fursa kwenye maafa

**JUMAMOSI** ya Novemba 16, Watanzania walianza siku kwa majonzi na hofu, baada ya jengo la ghorofa nne kuporomoka Kariakoo jijini Dar es Salaam na kuua watu 16 kwa taarifa za juzi jioni.

Jengo hilo limesababisha idadi kubwa ya watu kunaswa kwenye vifusi na bado kazi ya uokoaji inaendelea.

Kwa muda wa siku tano juhudi za kuwasaka manusura zinafanyika mchana na usiku huku serikali ikithibitisha vifo vya watu 16 na wengine 86 wamejeruhiwa na kupelekwa katika hospitali mbalimbali kutibiwa.

Hata hivyo, Waziri Mkuu Kasim Majaliwa, wakati akiongoza wananchi kuwaaga waliofariki katika tukio hilo, alionesha kusikitishwa na baadhi ya watu kuchukulia majanga hayo ya kitaifa kama mtaji wa kujipatia fedha kwa kuwachangisha watu fedha za kusaidia walioathirika.

Katika kuonesha hapendezwi na tabia hiyo, Waziri Mkuu, analitaka Jeshi la Polisi kumkamata Jennifer Jovin, maarufu kama Niffer, baada ya kuchangisha fedha kutoka kwa wananchi kwa madai ya kusaidia waathirika wa tukio hilo.

Pamoja na kutoa agizo hilo, alipiga marufuku kwa yeyote kuchangisha fedha katika matukio ya maafa, akieleza kazi hiyo inafanywa na serikali kupitia akaunti maalum inayosimiwa na kitengo cha maafa kilichoko chini ya ofisi yake.

Baada ya kauli hiyo, Jeshi la polisi lilitoa taarifa ya kukamata mtuhumiwa huyo, huku Jennifer mwenyewe akikiri kufanya kitendo hicho na kujitetea kuwa alifanya hivyo kwa nia njema na kwamba hakujua miongozo sahihi ya uchangishaji katika matukio ya maafa.

Hata hivyo, jambo linalowafanya Watanzania kupata tabasamu ni kuona serikali imeliona tatizo hilo ambalo limekuwa na pia kuonekana kero ndani ya jamii.

Maafa mengi yaliyotokea nyuma kama maporomoko ya Hanang, kuna baadhi ya watu na taasisi mbalimbali walichangisha fedha nyingi, lakini haikujulikana kama kweli ziliwasilishwa katika sehemu sahihi au ziliishia kwenye mikono na matumbo ya watu.

Ilikuwa jambo la kawaida kuona watu na taasisi hizo zikitangaza michango katika kurasa zao za mitandao ya kijamii au katika vyombo vya habari zikieleza kutaka kwenda kusaidia jamii zilizoathirika.

Hata hivyo, pamoja na kujipatia fedha nyingi za michango, hakuna mrejesho wa matumizi au uwasilishaji wake sehemu zilizotakiwa kwenda.

Kwa maana nyingine, hakuna aliyejua fedha hizo zimekwenda wapi, licha ya Watanzania wengi wenye tabia ya upendo na kujitoa kujitokeza kuchangia.

Waziri Mkuu kupiga marufuku uchangishaji fedha katika matukio hayo yanayogusa hisia za watu, ni sawa na kuweka asali kwenye kidonda kibichi kwani wengi walikuwa wakiumia ndani ya mioyo yao kutokana na kushindwa mahali pa kusemea.

Wachangishaji wengi ni watu wenye nguvu na wapo karibu na viongozi wa serikali, hivyo pengine jamii haikuona wakiguswa wala kuulizwa. Wengi wakaamini kuwa ni kwa kuhofia kuonekana kuwa kufanya hivyo sio uzalendo.

Si katika matukio ya maafa tu ambayo wananchi tunapigwa, hata katika misiba au ugonjwa kwa watu mashuhuri tumesikia malalamiko ya watu wanajiweka mbele kwa kusimamia michango na kisha kutoweka nayo.

Hiyo ndio jamii tunayokuwa nayo kwa sasa ambayo kimsingi imekuwa haina hofu ya Mungu na imejaa ubinafsi na kusaka mali kwa hali yoyote.

Waziri Mkuu kuliona hilo na kukemea hadharani, ni sawa na kutoa mwanga kwamba tunapoelekea sawa tunakwenda shimoni, hivyo tubadilike na kuuweka Utanzania mbele.

Wakati wa kurudi kule tulipotoka umewadia, kwani wenzetu wakipata matatizo tujitokeze kuwafariji badala ya kugeuza kuwa mtaji wa kujikusanyia fedha.

Tusisubiri tena kiongozi wa juu ajitokeze kukemea mambo kama haya, sisi wenyewe tunaweza kukomesha kwa kuacha kujitokeza kuchangia michango ambayo hatuna uhakika nayo kama inalenga kusaidia au kwenda kwenye mifuko ya watu ambao hawana utu.

# SUA yatenga bil. 1/- kila mwaka kuinua watafiti

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

CHUO Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA), kimeamua kutenga Shilingi bilioni moja kila mwaka kwa ajili ya kuinua watafiti wachanga ili wafanye utafiti kusaidia kutatua changamoto za jamii na taifa.

Rasi wa Ndaki ya Sayansi Asilia naTumizi (CoNAs), Dk. Geofrey Karugila, alisema hayo kwa niaba ya Makamu Mkuu wa Chuo hicho, Profesa Raphael Chibunda.

Dk. Karugila alimwakilisha Makamu Mkuu wa Chuo kuzindua Mradi wa mbinu shirikishi za wanafunzi na wakulima katika uvumbuzi na uhaulishaji wa maarifa na teknolojia za kilimo (AGRISPARK).

Alisema mradi huo ni matokeo ya maono makubwa ya Chuo Kikuu hicho katika kuinua watafiti wake hasa wachanga kwa kutenga fedha za ndani ili wafanye utafiti wa kusaidia kutatua changamoto za jamii na taifa.

"Hiyo ni sehemu ya matunda ya fedha hizo za serikali ambazo zimekusudia kusaidia kuleta ufumbuzi wa changamoto zinazowakabili Watanzania huku zikiwajengea uwezo watafiti wetu," alisema Dk. Karugila.

Dk. Karugila aliwataka watafiti kushirikiana na jamii kubuni mbinu zinazoweza kusaidia kuondoa changamoto zao ili jamii iweze kunufaika na kazi kubwa zinazofanywa nao badala ya kutumia fedha na rasilimali zingine na kuzalisha ubunifu ambao hautatumiwa na jamii.

Mtafiti Mkuu wa mradi huo, Dk. Philbert Nyinondi kutoka SUA, alisema mradi huo umekuwa wa kipekee kwa kuwa si tu unafadhiliwa na fedha za ndani bali unajibu moja kwa moja changamoto zinazoikabili jamii.

"Tunafanya tafiti ambazo tumefadhiliwa na wafadhili toka nje ya nchi, unapewa fedha kulingana na ajenda ya mtoa fedha au kitu anachokipenda," alisema Dk. Nyinondi.

Alisema utafiti unaofadhiliwa na fedha za ndani moja kwa moja inakwenda kugusa maisha ya watu kwa maana zinafanyia utafiti kitu au jambo ambalo moja kwa moja lina maslahi kama taifa kwa maendeleo ya nchi.

Alisema jambo lingine la mradi ni kuwashirikisha zaidi wanafunzi kwenye utafiti huo ili wanapomaliza wawe wanajua changamoto zinazowakabili wakulima kuanzia wanapoandaa shamba hadi kuvuna.

Dk. Nyinondi alisema mradi unalenga pia kuangalia jamii ya wananchi wanaozunguka Chuo Kikuu hicho inavyoweza kunufaika na matokeo yake ndio yatasababisha mradi kutoka na usambazwe nje ya Mkoa wa Morogoro au la.

Mtafiti mkuu mwenza wa Mradi huo, Dk. Nicholaus Mwalukasa, alisema mradi huo unafanyika katika halmashauri tatu za Mkoa wa Morogoro ambazo ni Manispaa ya Morogoro, Mvomero na Halmashauri ya Wilaya ya Morogoro.

Alisema utafiti wa awali uliofanywa kuangalia mbinu za ushirikishi za watafiti na wakulima katika uvumbuzi na uhaulishaji wa maarifa na teknolojia za kilimo umebaini kuwa zaidi ya asilimia 70 ya wakulima hawawashirikishwi katika hatua za awali za ubunifu na teknolojia.

Dk. Mwalukasa alisema kwa matokeo hayo inamaanisha watafiti wanahitaji kuwashirikisha wakulima zaidi katika hatua za awali za uundaji wa maarifa na maendeleo ya ubunifu ili kuhakikisha teknolojia za kilimo zinafaa zaidi, zinapokelewa kwa urahisi na kuwa endelevu.



Mwenyekiti wa Umoja wa Vijana wa Chama Cha Mapinduzi (UVCCM) mkoa wa Lindi, Twaiba Mpako (kushoto), akikabidhi fulana kwa Katibu wa Umoja huo, Esther Belbes mkoani humo juzi, kwa ajili ya wanachama wao, wazitumie kuhamasisha wananchi wajiandae kushiriki uchaguzi wa serikali za mitaa. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# 'Wanaopata majanga wanahitaji kupatiwa elimu afya ya akili'

**Na Christina Mwakangale**

WAKATI zikiwa zimepita siku nne tangu tukio la ghorofa kuporomoka mtaa wa Mchikichini na Msimbazi, Kariakoo, jijini Dar es Salaam na kusababisha vifo takribani 16 na majeruhi zaidi ya 80 kuokolewa, wito umetolewa na mtaalamu wa afya wa haja ya kujali afya ya akili.

Bingwa wa Afya ya Akili kutoka Hospitali ya Rufani ya Kanda Mbeya (MZRH), Dk. Raymond Mgeni, ameshauri mambo tisa ya kuzingatia baada ya matukio ya majanga, ikiwamo kutoa mafunzo, msaada maalum kwa wahudumu waliokuwa mstari wa mbele katika uokozi na kujikuta wakipata athari za kiakili.

Bingwa huyo akielezea zaidi kuhusu suala hilo, kwa Nipashe jana, alisema majanga yanaweza kutokea wakati wowote bila kujali yanaweza kumkuta mtu akiwa katika hali gani.

Alisema majanga kama ya moto, ajali, maporomoko, mafuriko yanaweza kujitokeza na mara nyingi kinachotakiwa haraka ni afya ya mwili, na kuisahau afya ya akili.

"Tunasahau upande wa athari za kiakili na kihisia wakati wa janga na baada ya janga hilo. Tunaweza kuunganisha nguvu katika kujumuisha tathmini ya afya ya akili, kwa mtu ambaye kapata janga wakati huo na baada ya kupita kwa janga.

Hapa inaweza kuhusisha manusura au hata waliojeruhiwa moja kwa moja. Msaada wa kisaikolojia una mchango wake mkubwa katika kupunguza athari za kiakili zinazokuja baada ya janga.

Tunaweza kuangazia mambo kadhaa katika kujenga hili hasa wakati wa majanga yanapojitokeza," alisema bingwa huyo na kuyaorodhesha yanayopaswa kuzingatiwa.

Dk. Mgeni ametaja utoaji wa huduma za haraka za kisaikolojia kwa waathirika pamoja na kutoa msaada wa kihisia na kuwasaidia waweze kuelewa hali wanazopitia kwa wakati huo.

Ameshauri kufanyika tathimini ya afya ya akili kwa waathirika ikiwa ni pamoja na kugundua dalili za awali za wasiwasi, maumivu badaa ya janga na kadhalika.

Pia, eneo la tatu anashauri utoaji na uendelezaji mafunzo kwa wahudumu wa kwanza wa uokozi ni muhimu hasa kwa vyombo vya dola, zimamoto, watumishi wa afya kuhusu athari za kiakili za majanga.

Bingwa huyo ametaja suala lingine ni uwapo wa makundi saidizi ya watu kuelezea hisia zao baada ya janga ili kupunguza athari zaidi za kiakili kutokana na majanga.

"Tano ni kutoa msaada wa zaidi kwa makundi maalumu wakati wa majanga mfano uokozi wa watoto, wanawake wajawazito, wazee, wenye ulemavu wa mwili na akili na makundi yote yaliyo katika hatari.

Suala la sita ni kukumbuka kutoa mafunzo au msaada maalum kwa wahudumu waliokuwa mstari wa mbele katika kusaidia uokozi na wakajikuta wakipata athari za kiakili kwa matukio hayo."

Eneo la saba kutoka kwa bingwa huyo, ni ushauri kuhusu ushiriki wa serikali na wadau wote muhimu katika uwapo wa sera za kitaifa kuhusu dharura, mipango na mafunzo ya mara kwa mara ya ukabilianaji wa aina mbalimbali za majanga.

Pia, ameshauri ufundishwaji wa mafunzo kwa umma hasa utoaji wa elimu wa namna ya kujitayarisha na dharura katika wigo wa afya ya akili.

"Majanga mengi huweza kuzua taharuki, wasiwasi mkubwa na kuacha kumbukumbu mbaya na za maumivu ambazo bila kushughulikiwa kunaweza kusababisha matatizo mengi yahusuyo na afya ya akili," anasema Dk. Mgeni.

Eneo la tisa anasema ni uwapo uhamasishaji na uendelezaji wa wadau wote ambao wataonesha utayari wa kufanya utafiti kuhusu athari za kiakili za majanga kwa makundi tofauti ya watu, aina ya janga na madhara ya janga lilivyosababisha.

Alisema, matokeo ya utafiti yasaidie kuboresha huduma za afya ya akili na saikolojia kuhusu majanga na kuisaidia katika jamii kwa kuyaangalia kwa wigo wa afya ya akili na kisaikolojia.

## KABWELA

FADHILI MOHAMED



# Kigogo TPA akana kuwapo kazini zabuni ilipopitishwa

**Na Kulwa Mzee**

ALIYEKUWA Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA), Mhandisi Madeni Kipande, amekana kuwapo kazini wakati zabuni ya Enterprises Planning Resources (ERP) inapitishwa.

Kipande amedai kuwa wakati huo hakuwapo kazini kama Mkurugenzi Mkuu wa TPA kwa kuwa alikuwa tayari amesimamishwa kazi. Alidai kuwa zabuni hiyo ilipitishwa na mtu mwingine aliyeteuliwa kuchukua nafasi yake.

Mhandisi Kipande alidai hayo jana katika Mahakama Kuu Divisheni ya Rushwa na Uhujumu Uchumi wakati upande wa Jamhuri ukimsomea mashtaka na maelezo ya awali yanayomkabili na wenzake, mbele ya Jaji Godfrey Isaya.

Washtakiwa wengine katika shauri hilo ni aliyekuwa Mkurugenzi wa Ununuzi, Mashaka Kisanta, Mwenyekiti wa Bodi ya Ununuzi, Casmir Lujegi na Kaimu Mkurugenzi wa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano, Kilian Chale.

Upande wa Jamhuri ukiongozwa na Wakili wa Serikali Petro Ngasa, ulianza kuwasomea washtakiwa mashtaka yanayowakabili.

Alidai katika shtaka la kwanza la washtakiwa wote wanadaiwa kuongoza genge la uhalifu, inadaiwa kati ya Januari 2014 na Machi 2019 maeneo ya TPA, waliunda genge hilo na kupata idhini ya kutangaza zabuni ya serikali namba AE/016/2014-15/CTB/G/39 na kusababisha Kampuni ya Twenty Third Century System Tanzania Ltd kupata Dola za Marekani 1,857,908.40.

Katika shtaka la pili, inadaiwa kati ya Januari Mosi na Februari 28, 2015 wakiwa maofisa wa TPA, walitumia madaraka yao vibaya kwa kutangaza zabuni namba AE/016/2014-15/CTB/G/39 bila kuwepo kibali kutoka Bodi ya Zabuni kwa nia ya kujipatia Dola za Marekani 1,857,908.40.

Katika shtaka la mwisho, washtakiwa wanadaiwa kati ya Januari Mosi, 2015 na Machi 21, 2019 maeneo ya TPA, wakiwa na nia ovu, walisababisha hasara ya Dola za Marekani milioni 1.8.

Akisoma maelezo ya awali, Wakili Ngasa alidai nyaraka za zabuni ziliwasilishwa katika Bodi ya Zabuni ya TPA Januari 20, 2015 na bodi haikupitisha zabuni hiyo kwa sababu ya upungufu uliokuwapo.

"Bodi ilielekeza kuwa zabuni isitangazwe hadi apatikane mshauri wa kupitia," alidai Ngasa.



Mkurugenzi wa Chemba ya Wafanyabiashara Wanawake Tanzania (TWCC), Mwajuma Hamza, akizungumza wakati wa tuzo za Shirika la Viwango Tanzania (TBS) kwa wazalishaji waliozingatia ubora, jijini Dar es Salaam, jana. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

Alidai mshtakiwa wa pili, Mashaka, aliandika barua kuomba kupitisha nyaraka za zabuni kwa ajili ya usambazaji ya uanzishaji wa mafunzo.

Wakili Ngasa alidai kuwa Januari 26, 2015 Mashaka alimwandikia barua mshtakiwa wa tatu, Chale, akionesha kutofurahishwa na uamuzi wa bodi kutopitisha zabuni na akamweleza mshtakiwa Kipande atangaze zabuni hata kama haijapitishwa.

Ilidaiwa kuwa zabuni ilitangazwa bila kupitishwa na Bodi ya Zabuni na mshtakiwa Lujegi alitia saini nyaraka za zabuni zilizokwenda kwa waombaji wa zabuni bila kupitishwa na bodi.

Mshtakiwa Kipande anadaiwa kupitisha zabuni hizo kutangazwa na zabuni ilipewa Kampuni ya Twenty Century kwa thamani ya Dola za Marekani 6,635,387.16.

"Mshtakiwa Mashaka na Chale waliandaa mkataba na kupuuzia maelekezo ya timu iliyochunguza.

"Kati ya mwaka 2014 na mwaka 2020 maeneo ya TPA na maeneo mengine ya Dar es Salaam, kwa makusudi walitangaza zabuni ya Enterprises Planning Resources (ERP),"alidai Wakili Ngasa.

Washtakiwa hao wanadaiwa walitangaza zabuni hiyo, bila kupata kibali cha Bodi ya zabuni ya TPA na kushindwa kufuata kanuni za zabuni, hivyo kutoa malipo ya awali ya asilimia 40 bila idhini ya bodi hiyo, jambo lililosababisha TPA kupata hasara ya Dola za Marekani milioni 1.8.

Washtakiwa walikubali taarifa zao binafsi na kukana maelezo yote kuhusu mashtaka yanayowakabili.

Mshtakiwa Kipande alikana kwamba wakati wa mchakato wa zabuni kupitishwa hakuwa mkurugenzi na kwamba zabuni ilitiwa saini akiwa tayari amesimamishwa kazi, hivyo aliyepitisha ni mtu mwingine aliyechukua nafasi yake.

***Kwa maoni kuhusu habari hii: Piga/sms / WhatsApp : +255 677 020 701***
***Email: customerrelations@guardian.co.tz***


**TANGAZO LA MKUTANO MKUU WA MWISHO WA WANAHISA WA KAMPUNI YA**

**AMANDI E.A LIMITED**

**Cheti cha Usajili No. 97727**

Sheria ya Makampuni, 2002 (Kifungu 334 (1))

Umma na wahusika wanafahamishwa kutakua na mkutano mkuu wa mwisho wa wanahisa wa kampuni AMANDI E.A LIMITED, yenye usajili namba 97727 kitakachofanyika tarehe 2/12/2024 ofisini kwa mfilisi saa 4:30 asubuhi ambapo mfilisi atatoa hesabu ya kufungwa kwa hiari kwa kampuni.

| | |
|---|---|
| Mfilisi | JOHNPAUL THADEI MWAKILASA |
| Amwani ya Mfilisi | 368 MSASANI ROAD<br>MIKUMI HOUSE<br>OYSTERBAY<br>P.O BOX 9673<br>DAR ES SALAAM<br>TANZANIA |
| Tarehe ya kuchaguliwa | 15 May 2023 |
| Amechaguliwa na | WAMILIKI WA KAMPUNI |

Sahihi .................................................... Tarehe: 1/11/2024

Jina: JOHNPAUL THADEI MWAKILASA


# Masharti mapya leseni uchimbaji madini

**Na Maulid Mmbaga**

SERIKALI imeweka utaratibu mpya kwa kampuni zote za madini zitakazohitaji leseni za uchimbaji, kufanya shughuli za uongezaji wa thamini nchini ili kutengeneza ajira na ukuaji wa pato la taifa.

Akizungumza jana Dar es Salaam katika mkutano wa Kimataifa wa Uwekezaji na Madini wa mwaka huu, Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, alisema Tanzania ni moja ya nchi chache za Afrika zenye uzalishaji mkubwa wa madini lakini bado hainufaiki ipasavyo na rasiliamli hiyo kwa sababu uongezaji thamani kwa kiasi kikubwa unafanyika nje.

Kwa sababu hiyo, alisema taifa linakosa manufaa mapana kwenye mnyororo wa thamani ikiwamo ajira na mapato ambayo yangepatikana endapo madini yangeongezewa thamani nchini.

"Kwa kutambua manufaa makubwa ya kijamii na kiuchumi yanayotokana na uongezaji thamani madini kufanyika ndani ya nchi, serikali inaendelea kuweka mazingira wezeshi ikiwamo kufanya mapitio ya sera, sheria, kanuni na miongozo mbalimbali ambayo inabainisha changamoto zilizoko ili kushughulikia hasa kwenye eneo la uongezaji thamani.

"Lengo la serikali ni kuhakikisha sekta ya madini inaendelea kutoa mchango wake hasa katika ukuaji wa uchumi wa nchi kwa kuona inachangia zaidi ya asilimia 10 katika pato la taifa ifikapo 2025. Mchango katika sekta hii umekua kwa sababu ya ongezeko la asilimia 7.3 mwaka 2021 hadi tisa," alisema.

Majaliwa alisema serikali imechukua hatua ya kuhakikisha wawekezaji wakubwa na wadogo katika sekta ya madini wanaendesha shughuli zao kwa tija na kuwezesha mazingira wezeshi ya uwekezaji na upatikanaji wa teknolojia unaimarika.

Alisema hiyo itakwenda sambamba na uboreshaji wa miundombini mbalimbali ambayo serikali imeamua kuiimarisha kwa lengo la kuvutia na kuwezesha uwekezaji kuleta faida kwa kila mwekezaji, ikiwamo kuongeza uwezo wa nishati ya umeme kwenye gridi ya taifa na kuimarisha njia za usafirishaji kama barabara, reli, bandari na anga kwa kuongeza ndege zaidi.

Pia alisema serikali pia imejikita katika kuimarisha huduma za masoko kila mkoa na vituo vya ununuzi wa madini kwa kuviongezea uwezo kila maeneo ambayo kunachimbwa thamani hiyo na kwamba kufikia sasa wana masoko 44 katika mikoa mbalimbali nchini na vituo 103.

"Kupitia masoko na vituo hivyo, kumekuwako na mzunguko mzuri wa ukusanyaji wa madini hasa katika mwaka 2023/24 madini yenye thamani ya Sh. trilioni 2.59 yaliuzwa kupitia masoko na kuwezesha serikali kukusanya Sh. bilioni 180.

"Pia serikali imeongeza bajeti ya Wizara ya Madini kutoka Sh. bilioni 89 mwaka 2023/24 mpaka Sh. bilioni 231.9 kwa mwaka wa fedha 2024/25. Ongezeko hili linalenga kuboresha mambo mbalimbali ya kisekta ikiwemo kuboresha huduma hasa kwenye Taasisi ya Jiolojia na Utafiti wa Madini, kufanya utafiti wa kina na kutoa matokeo yatakayowanufauisha Watanzania," alisema Majaliwa.



## TARURA kufungua barabara za kilomita 109 wilaya tatu

**Na Mwandishi Wetu,** MANYARA

WAKALA ya Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA) mkoani Manyara, imepanga kufungua barabara mpya zenye urefu kilomita 109 katika Wilaya za Mbulu, Simanjiro na Babati.

Kwa mujibu wa Kaimu Meneja wa TARURA, Salim Bwaya, alisema jana kuwa barabara hizo zimepangwa kufunguliwa katika mwaka wa fedha 2024/2025.

Bwaya alisema kilomita hizo za barabara, zitawanufaisha wananchi na kuwaletea manufaa ya kiuchumi na kijamii kwa kuwarahisishia kupata huduma za kijamii kwa urahisi.

"Mwaka huu wa fedha tuna mpango wa kufungua barabara katika Wilaya ya Mbulu (kilomita 46), Simanjiro (kilomita 41) na Babati (kilomita 22).

"Vilevile, ujenzi huo utajumuisha ujenzi wa barabara za lami (kilomita 11.7), changarawe (kilomita 251.4) pamoja na matengenezo ya barabara za udongo (kilomita 385) na ujenzi wa vivuko vipatavyo 104."

Kadhalika, alisema licha ya kufungua kilomita hizo za barabara hali ya mtandao wa barabara katika maeneo mengi katika mkoa huo ni nzuri kwani unapitika katika kipindi chote cha mwaka.

Aidha, alisema kuwa utekelezaji huo unaendelea kutokana na ongezeko la bajeti katika mkoa huo ambapo kwa sasa bajeti yao imepanda mara tatu kutoka Sh. bilioni 6.788 mwaka 2021 hadi kufikia Sh. bilioni 19.7 mwaka 2024/2025.

"Hili ni ongezeko kubwa na limetuwezesha kuongeza ubora wa mtandao wetu wa barabara, kwa kuwa mwaka 2021, tulikuwa na barabara za lami kilomita 17 na sasa tuna kilomita 33.03, barabara za changarawe kutoka kilomita 950 hadi kufikia kilomita 1980 na kiwango kinachobaki ni kiwango cha udongo," alifafanua.

...Tunaishukuru serikali kwa kutuongezea bajeti mara tatu ya bajeti ya awali na hivyo tumeweza kuongeza madaraja ya mawe kutoka daraja (1) mwaka 2021 hadi kufikia madaraja (10)."

Pia, alisema wameweza kuongeza madaraja madogo na ya kati kutoka 283 hadi 530 vile vile madaraja makubwa yameongezeka kutoka madaraja (2) mwaka 2021 hadi kufikia madaraja (28) kwa mwaka huu wa fedha.

Kwa upande wa mabadiliko ya tabianchi na utunzaji wa miundombinu ya barabara, alisema wanaendelea kutoa elimu kwa jamii kuhusu madhara yanayosababishwa na uharibifu wa miundombinu hasa mifereji, kung'olewa kwa alama za barabara na uvamizi wa hifadhi za barabara kwa shughuli za kiuchumi.

Alisema vilevile wanatoa elimu ya umuhimu wa kupanda miti na kutunza mazingira na kuacha kufanya shughuli zingine za kibinadamu kwenye hifadhi za misitu na kwenye vyanzo vya maji.

Hata hivyo, alitoa wito kwa wananchi kuendelea kutunza miundombinu ya barabara kwa kuzingatia sheria na kanuni zake kwani serikali inawekeza fedha nyingi kwenye miundombinu ya barabara, hivyo ni wajibu wao kuitunza ili waendelee kunufaika nayo kwa muda mrefu.

Mkazi wa Babati, Bakari Sanka, alisema mkoa wao unapokea mazao mengi kutoka vijijini, hivyo kukamilika kwa ujenzi wa madaraja na miundombinu mingine imewanufaisha wananchi wengi na hivyo shughuli zao za uzalishaji zinaendelea kama kawaida.

# Mataifa yanayolima kahawa Afrika kukutana Tanzania

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

TANZANIA imechaguliwa kuwa mwenyeji wa mkutano wa kimataifa kahawa Afrika, utakaoshirikisha mataifa 11 yanayolima kwa wingi zao hilo.

Mkurugenzi Mkuu wa Bodi ya Kahawa (TCB), Primus Kimaryo, alieleza hayo juzi katika Mji wa Moshi, wakati akiwasilisha taarifa ya bodi hiyo kwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo.

Alisema nchi hizo zimekubaliana kufanya mkutano huo katika Mji wa Moshi, mkoani Kilimanjaro, mahali ambako ni kitovu cha zao hilo la kimkakati.

Alisema kwa mwaka huu, menejimenti yake imepanga kuzalisha miche bora ya kahawa 22,628,919 sawa na asilimia 113.1 ya lengo lililowekwa la kuzalisha miche milioni 20 na kuisambaza kwa wakulima.

Katika mpango wa kuimarisha uzalishaji wa zao hilo, Kimaryo alisema TCB inatekeleza mradi wa uchimbaji wa visima 10 kwa ajili ya umwagiliaji kwenye mashamba ya kahawa ya Mbozi, mkoani Songwe.

Aidha, alisema zao hilo hivi sasa linakabiliwa na changamoto ya konokono kuathiri majani ya kijani ya zao hilo lenye soko kubwa duniani.

"Malengo yetu ni kuimarisha pia mashamba makubwa hekta 4,000, ambapo kati ya hizo, eneo lenye ukubwa wa hekta 358 limepatikana Wilaya ya Karagwe, Kagera," alieleza.

Alisema mfumo wa masoko wa direct export, umeisaidia Tanzania kuuza kahawa yake nje ya nchi kwa asilimia 80.

Vilevile alisema fedha iliyoingia moja kwa moja kwa wakulima kwa mwaka 2023 kutokana na zao hilo ni Dola za Marekani 235.




Waziri Mkuu mstaafu, Mizengo Pinda, akifungua jiwe la msingi la maadhimisho ya Miaka 30 ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania (OUT), chuoni hapo, Kinondoni, Dar es Salaam juzi. Kushoto ni Makamu Mkuu wa Chuo hicho, Prof. Elifas Bisanda. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Madaktari bingwa Manyara waanzisha kliniki maalum

**Na Jaliwason Jasson,** BABATI

MADAKTARI bingwa 15 katika Mkoa wa Manyara, wameanzisha kliniki maalum ya huduma kwa wananchi wa eneo hilo.

Huduma hiyo itazunguka katika halmashauri zote za mkoa huo, ili kuwaepushia kutumia gharama kubwa kufuata huduma hiyo Hospitali ya Rufani ya Kanda ya Kaskazini ya KCMC.

Mbali na kliniki hiyo, pia serikali mkoani humo imetangaza neema ya ujio wa madaktari bingwa wengine kutoka Shirika la Roberts and Friends la nchini Marekani, Februari mwaka ujao.

Uamuzi wa kuanzisha kliniki hiyo ya madaktari bingwa wazawa, ilitangazwa jana na Mkuu wa Mkoa huo, Queen Sendiga.

Alisema wameamua kuanza kuwatumia madaktari bingwa wa ndani ya mkoa ili waweze kusaidia kutoa huduma kwa wananchi kuliko kuwasubiri madaktari bingwa na bobezi wanaotolewa na Rais Samia Suluhu Hassan wanaozunguka nchi nzima.

"Mkoa umeona ni vyema kwa kutumia vyanzo vya ndani vya mapato kwenda kutibu wagonjwa katika wilaya zote kwa kuwatumia madaktari bingwa wetu wa mkoa,"alisema Sendiga

Aidha, alisema wameamua kuanzisha kliniki hizi za madaktari bingwa wa ndani kutoa huduma kila wilaya kwa kuwa kila halmashauri ina Hospitali ya Wilaya na vipo vituo vya afya ambavyo vina vifaa tiba vya kutosha.

Mkuu huyo alisema kazi ya kuwatumia madaktari bingwa hao itakuwa endelevu ambapo itahusisha madaktari wa upasuaji, magonjwa ya wanawake na uzazi, macho, shinikizo la damu na sukari pamoja na daktari bingwa wa watoto.


Sendiga alisema kliniki hiyo itaanza Novemba 19 mpaka 22 katika Wilaya ya Simanjiro ambapo zitawapunguzia gharama wananchi za kusafiri kufuata matibabu.

"Tunaenda kuongeza uchunguzi wa magonjwa sugu ambayo yanawakabiri wananchi na tutawajengea uwezo wataalamu wetu wa afya katika halmashauri,"alisema Sendiga

Katika hatua nyingine, alisema Shirika la Roberts and Friends la nchini Marekani litaleta madaktari bingwa 20 Februari mwaka 2025 mkoani hapa ili kutoa huduma ya kibingwa na bobezi kwa wananchi.

Alisema madaktari hao watakuja na vifaa tiba vyao ili kutoa huduma japo watatumia na vifaa vya ndani watakavyovikuta.

Mganga Mkuu wa Mkoa huo, Dk. Andrew Method, alisema madaktari bingwa wa ndani watakuwa mkombozi kwa wananchi kwa kuwa watafika kila wilaya na watawapa ujuzi madaktari wa wilaya husika.



# BoT yatahadharisha ukopaji holela kwenye taasisi

**Na Marco Maduhu,**
MWANZA

BENKI Kuu ya Tanzania (BoT) Tawi la Mwanza limetoa tahadhari kwa wananchi kuhusu ukopaji holela kwenye taasisi zenye masharti magumu, kuwataka kukopa kwenye taasisi zilizo na leseni.

Meneja Msaidizi Idara ya Uchumi kutoka BoT, Issa Pagali, alisema hayo wakati wa mafunzo ya masuala ya fedha kwa waandishi wa habari.

Alisema ili wananchi waepukane na mikopo ambayo siyo rafiki kwao 'kausha damu' ni vyema wakakopa fedha kwenye taasisi za huduma ndogo za kifedha ambazo zimepatiwa leseni na BoT, zenye riba elekezi isiyozidi asilimia 3.5 kwa mwezi.

Alisema kupitia kwenye tovuti ya BoT imethibitisha taasisi zote za kifedha ambazo zimepewa leseni na benki hiyo, ambapo wananchi wanapaswa kuingia na kuona taasisi hizo.

"Utoaji wa leseni kwa watoa huduma ndogo za kifedha daraja la pili tumeshatoa leseni zaidi ya 2,100 na maombi yapo mengi sana," alisema Pagali.

Aidha, alisema kwa mtoa huduma ndogo ya kifedha ambaye ana leseni ya BoT akikiuka masharti ya leseni hiyo na kutoza riba kubwa adhabu yake kubwa ni kufutiwa leseni.

Alisema mipango ya baadaye ni kuokoa wananchi na mikopo kausha damu, kutoa elimu kwa umma kupitia vyombo vya habari kuhusiana na umuhimu wa kuelewa vigezo na masharti ya mikataba ya ukopeshaji na kupatiwa nakala ya mkataba uliosainiwa.

Alitaja mipango mengine kuwa ni kuwaelimisha wananchi juu ya athari za kukopa mikopo kwa watoa huduma ndogo za kifedha wasio na leseni kutoka BoT pamoja na kujenga mfumo wa uwazi juu ya riba.

Alisema benki hiyo pia imeidhinisha utekelezaji wa kampeni dhidi ya mikopo umiza isemayo zinduka, 'usiumizwe kopa kwa maendeleo' ambayo itatolewa kupitia vyombo mbalimbali vya habari.

Mkurugenzi wa BoT Tawi la Mwanza, Gloria Mwaikambo, aliwataka wananchi pia wanapoingia kwenye taasisi ndogo za watoa huduma za kifedha kwa ajili ya kukopa, kuangalia leseni zao ambazo hubandikwa ukutani.

Pia aliwataka kusoma mikataba ya mikopo na riba na kuchukua nakala ya nyaraka aliyokopea fedha.



Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Anamringi Macha (kushoto), akiwa na Mkuu wa Wilaya ya Kishapu, Joseph Mkude, baada ya kukamata mifuko 437 ya mbegu za pamba zikiwa kwenye gari aina ya Fuso lenye namba za usajili T.618 DRJ, katika kijiji cha Nyasamba, wilayani Kishapu juzi, zilizokuwa zikitoroshwa kwenda kuuzwa maeneo mengine. **PICHA: MARCO MADUHU**

# Maofisa waagizwa kuwatembelea watumishi wa umma kusikiliza kero

**Na Elizabeth Seleman,**
SENGEREMA

MWENYEKITI wa Halmashauri ya Wilaya Sengerema mkoani Mwanza, Yanga Makanga, amewaamuru maofisa wa idara mbalimbali katika halmashauri hiyo kushuka chini kwa watumishi wa umma kusikiliza na kutatua kero zinazowasibu.

Alitoa agizo hilo juzi katika kikao cha baraza la madiwani na kuwataka maofisa elimu, afya pamoja na wakuu wa idara mbalimbali kuhakikisha wanatenga muda wa kukutana na watumishi hao na siyo kukaa ofisini.

Alisema maofisa elimu msingi na sekondari wanatakiwa kwende shuleni kusikiliza matatizo ambayo walimu wanakutana nayo na kuyatatua na kama yapo juu yao watoe taarifa sehemu husika na siyo kukaa ofisini.

Kadhalika, alimwagiza Mganga Mkuu wa Halmashauri kwenda katika vituo vyote vya afya kufuatilia na kusikiliza ni matatizo waliyonayo madaktari na wauguzi katika vituo vyao vya kazi ili yatatuliwe na kuwasaidia kutoa huduma bora.

"Halmashauri imepokea fedha nyingi kupitia sekta ya maji, barabara, afya pamoja na elimu na kupokea watumishi 104 wa idara ya afya na zaidi ya Sh.milioni 200 zimelipwa kufuatia malipo ya huduma ya ushuru hapa Sengerema hivyo ni vyema kuhakikisha wananchi wanapata huduma stahiki," alisema Yanga.

Mbunge wa Sengerema, Khamis Tabasamu alisema kupitia fedha za mfuko wa jimbo, mapato ya ndani na fedha za wadau zimetumika kujenga uwaja wa mpira wa miguu uliopo Mnadani.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Sengerema, Binuru Shekidele, alisema amejipanga na wakuu wa idara zote kusimamia miradi yote inayotekelezwa hapo likiwamo jengo la utawala linalogharimu zaidi ya Sh.bilioni 1.3 na kuhakikisha inakamilika kwa wakati pasipo kuchelewesha maendeleo ya wananchi.

## Ridhiwani ataka wahitimu elimu ya juu kuwa wabunifu

**Na Neema Emmanuel,** MWANZA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Ridhiwani Kikwete amewataka wahitimu wa Chuo cha Elimu ya Biashara (CBE) Kampasi ya Mwanza kutumia elimu yao kubuni mbinu mbadala kujiingizia kipato na siyo kusubiri kuajiriwa.

Alitoa kauli hiyo juzi wakati wa mahafali ya 59 ya chuo hicho na ya 17 kwa Kampasi ya Mwanza na kueleza kuwa kila mmoja ana njia ya kuibadilisha dunia.

Hivyo alisema ni vyema wajikite katika ujasiriamali na uvumbuzi na kutokukata tamaa kwani ndio ufunguo wa maisha yao.

"Kwa miaka mingi mmetafuta maarifa, ujuzi na uelewa mlionao kautumie kujenga maisha yenu na jamii kwani mnauwezo wa kubuni mbinu mpya ili kuleta mabadiliko na kuunda suluhu katika matatizo ya jamii, kiuchumi na mazingira huku mkizingatia vitu muhimu ambavyo ni ubunifu, uvumilivu na dhamira ya kubadilisha dunia na kutamani kuwa bora," alisema Ridhiwani.

Naibu Katibu Mkuu, Wizara ya Viwanda na Biashara, Balozi Dk. John Simbachawene alieleza kuwa serikali imezindua sera mpya ya biashara ya mwaka 2024 ambayo inasisitiza urahisi wa biashara, kupunguza vizuizi na kusaidia wajasiriamali hasa vijana na wanawake.

Balozi Simbachawene alisema sera hiyo inalenga kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji.

Mkuu wa CBE, Prof. Edda Lwoga alisema wanaendelea kujikita katika kukuza taaluma, utafiti na utoaji wa ushauri wa kitaalamu na kuendeleza ubora katika elimu.

Aidha, aliishukuru serikali kwa kuwatatulia tatizo la umeme mdogo chuoni hapo na kuwafungia transifoma ya kilovoti 300 ambayo imesaidia kuboresha mazingira bora kwa suala la umeme na maji ambayo yanawezesha wanafunzi kuwa na mazingira mazuri ya kujifunza.

Makamu Mwenyekiti wa Bodi ya Uongozi wa CBE, Dk. Kennedy Hoseah, alisema kuwa bodi imehakikisha mifumo ya utawala inazingatia uwazi na uwajibikaji katika maamuzi yote na imekuwa mstari wa mbele kuboresha mitaala kwa wakati ili kusimamia ubora wa elimu.

Mmoja wa wahitimu, Joshua Matiku alisema watatumia vyema maarifa waliyoyapata kwa uaminifu, uadilifu ili kukuza utu mahali popote watakapotumika.

Alisema hawatatumia maarifa hayo katika namna yoyote ambayo ni hatarishi kwa jamii na taifa bali watayatumia kuleta mabadiliko chanya na yenye tija.



Ukurasa 12

**Uturuki kushambulia penye ukame Syria, milioni moja walia na maji**



Ukurasa 13

Kampeni uchaguzi serikali za mitaa wanawake wachangiana fedha


# siasa

JUMATANO NOVEMBA 20, 2024

Nipashe

HABARI BORA NA KAMILIFU




Ukurasa 14

**FAYE NA ONKO**

**Hawakamatiki Senegali wapata ushindi wa kishindo**

# Wabunge viti maalum wanapoambiwa uchaguzi mkuu 2025 waende jimboni

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

ZANZIBAR ina safari ndefu kufikia azma ya azimio la Maputo linaloangazia uwakilishi wa usawa wa kijinsia wa uwiano wa 50/50 barani Afrika kwenye medani za kisiasa na uongozi wa umma.

Idadi ya wawakilishi wanawake wakuchaguliwa katika majimbo kwenye uchaguzi mkuu wa mwaka 2020 si kubwa hivyo wanahitaji waongezeke.

Kwa mujibu wa takwimu za baraza la wawakilishi lina wajumbe 78 kati ya hao wanawake 29 na wanaume 48.

Kwenye idadi hiyo, wanawake wawakilishi kutoka uchaguzi mkuu majimboni ni nane na wakati wanaume ni 42, wanawake wa viti maalum 18 na wajumbe wa kuteuliwa na rais wanane.

Mwaka 2025 ni uchaguzi mkuu, hivyo ni vyema idadi ya wanawake ikaongezeka katika nafasi za uongozi ikiwamo udiwani, uwakilishi na ubunge wa kuchaguliwa majimboni badala ya wanawake kutegemea viti maalum.

Na huo ndiyo wakati ni huu kwa wabunge, wawakilishi na madiwani kupitia viti maalum wanawake, watoke na kuungana na wanawake wengine kuwania katika majimbo ya uchaguzi.

Wafike huko kupambana na yeyote kwa kuwa tayari wameshapata uzoefu wa kutosha hivyo kuwapa nafasi wanawake wengine washike nafasi zao.

Uwalikishi wa wanawake kupitia viti maalum si uwakilishi wa kudumu bali ni nafasi za kujiandaa kisiasa, kujipima lakini pia za kupata uzoefu na kutumikia wananchi.

Kwa kuwa wawakilishi na wabunge wa viti maalum wameshapata mwanga, upeo na maarifa ya kazi hizo, hivi sasa yatosha waende na kwenda kuchuana kwenye majimbo ya uchaguzi.

Wapo ambao wamekaa kwenye nafasi hizo kwa miaka mitano, 10 na wengine hadi vipindi vinne. Wawakilishi, wabunge na madiwani hao wajiondoe na kwenda majimboni.

Kila mtu anajua kuwa licha ya kupata uzoefu, maarifa na ujuzi wa kisiasa, wameshajua mbinu za kupata ushindi na jinsi walivyojijenga katika jamii.

Mahusiano, ushirikiano na maelewano yao katika majimbo, kati ya wananchi yatakuwa yameimarika sana hivyo ni wazi watakuwa na ubavu wa kuwania nafasi katika majimbo ifikapo 2025.

Mwanahamis Kassim ambaye sasa ndiye mbunge wa jimbo la Magomeni Zanzibar, amewahi kuwa mbunge wa viti maalum kwa miaka mitano bungeni, ameamua kuwania uongozi jimboni na kushinda katika uchaguzi wa mwaka 2020.



Wawakilishi wa viti maalum wakiwa kwenye kikao cha Baraza la Wawakilishi Chukwani Zanzibar, kutoka kushoto ni Zainab Abdallah Salum, Mwanaidi Kassim na Salma Mussa Bilali. **PICHA: RAHMA SULEIMANI**

Uthubutu na uwezo wake umemfanya kupambana na kushinda wanaume waliokuwa wakipambana naye kwenye nafasi hiyo lakini kura zilimiminika na kulitwaa jimbo hilo.

Kwa mfano huo na mengine kuna wabunge, wawakilishi na madiwani kadhaa ambao kutokana na kuchapakazi katika kutumikia nafasi hizo, tunaamini wakiamua kwenda majimboni lazima washinde.

### VING'ANG'ANIZI

Sababu za kung'ang'ania viti maalum, zinatajwa na mwakilishi wa jimbo la Kiwengwa, Asha Abdallah Mussa, anayesema umefika wakati sasa wa wanawake kujikita majimboni kuwania uongozi badala ya kutegemea viti maalum.

Anasema hofu, woga, kutojiamini na mifumo dume ndiyo inayosababisha wanawake wengi kugombea nafasi za uongozi majimboni na nafasi hizo kuwaachia wanaume.

"Si kwamba wanawake hatuwezi kupambana na wanaume kugombea nafasi za uongozi majimboni, ni woga na hofu tu tuliyokuwa nayo. Tuwe na uthubutu wa kugombea majimboni ili kuwa na uwiano katika vyombo vya maamuzi," anasema.

Anasema wanawake wengi wakati wa uchaguzi mkuu hujikita hasa kwenye viti maalum kuliko nafasi za majimbo kwa sababu kwenye majimbo huwaogopa wanaume katika kushindana nao.

"Ukiangalia majimboni wapiga kura wengi ni wanawake lakini changamoto iliyopo ni mifumo dume. Yapo baadhi ya maeneo mifumo dume hiyo imeanza kuondoka na nafasi katika vyombo vya maamuzi ikiwemo baraza la wawakilishi imeongezeka kwa wanawake waliochaguliwa majimboni ikilinganishwa na miaka iliyopita," anasema.

Asha ambaye ni mwanamke wa kwanza kwa nafasi ya uwakilishi katika jimbo la Kiwengwa, anasema wanawake wapiga kura majimboni wana imani na wanawake katika kuwaongoza.

"Hata wanaume waliopo majimboni wanatuamini wanawake, na tunasema wanawake hatutarudi nyuma na wakati ukifika tutakwenda kupambana nao kuchukua fomu kugombea nafasi za uongozi majimboni kushiriki uchaguzi mkuu 2025."

Mwakilishi wa jimbo la Fuoni, Yussuf Hassan Iddi, anasema tatizo kubwa la wanawake kung'angania viti maalum kuliko kwenda majimboni, wanahisi kama kuna ugumu fulani majimboni.

Anasema ni suala la uthubutu hakuna ugumu kwa sababu wakijaribu wanaweza na wapo wawakilishi na wabunge wanawake ambao wanahudumia katika majimbo ya uchaguzi.

"Kwa mfano katika majimbo yuko Mtumwa Peya jimbo la Bubwini, Asha Abdallah Mussa Kiwengwa na wengine na hawa ukiwauliza vipi unaweza kwenda viti maalum kugombea watakuambia hawawezi maana huko nako kuna changamoto zake na wameshazowea majimboni," anasema mwakilishi huyo.

Aidha, anasema kuna changamoto kati ya wanawake wenyewe, kushindwa kuungana mkono hasa ikizingatiwa kuwa katika majimbo ya uchaguzi asilimia kubwa ya wapiga kura ni wanawake, hivyo anapotokezea mgombea mwanamke kumuunga mkono ili kufikia asilimia 50 kwa 50 katika vyombo vya maamuzi ikiwemo Bunge na Baraza la Wawakilishi.

INAENDELEA UK. 12

# Uturuki kushambulia penye ukame Syria, milioni moja walia na maji

• Wafuata kilomita 20; awali walishapatwa na tetemeko...



Hali halisi ya shida ya maji maeneo ya ukame, Syria. **PICHA: MTANDAO**

**Na Mwandishi Wetu**

INAELEZWA kuwapo mashambulizi ya anga kutoka Uturuki katika eneo lililokumbwa na ukame Kaskazini- Mashariki mwa Syria, yamesababisha uhaba wa upatikanaji wa umeme na maji kwa zaidi ya watu milioni moja.

Sasa wataalamu wanasema, huenda kuwapo ukiukaji wa sheria za kimataifa unaofanywa na washamhuliaji hao, tangu Oktoba mwaka 2019 hado kufika Januari mwaka huu.

Ni ushambulizi unaotekelezwa katika maeneo yenye mafuta, mitambo ya gesi na vituo vya umeme yanayoshikiliwa na jamii za Wakurdi huko Kaskazini na Mashariki mwa Syria.

Pia, mashambulizi hayo yanatajwa kuongeza hali mbaya ya kibinadamu katika eneo linalokumbwa na vita vya wenyewe vilivyodumu kwa miaka mingi, pia ukame mkubwa kwa miaka minne unaochangiwa na mabadiliko ya tabianchi.

Maji yantajwa yalikuwa kidogo, mashambulizi dhidi ya miundombinu ya umeme mwezi Oktoba mwaka jana yalikatisha umeme na kukatisha maji katika kituo kikuu cha maji cha eneo hilo, huko Alouk na hakifanyi kazi tangu wakati huo.

Serikali ya Uturuki inatajwa ililenga vyanzo vya mapato vya vikundi vya Wakurdi vinavyotaka kujitenga ambavyo vinahesabiwa kuwa ni vikundi vya kigaidi.

In ataja mahali hapo panajulkana kuna ukame na kuongeza kuwa usimamizi mbovu wa maji na miundombinu umesababisha hali kuwa mbaya zaidi.

Zaidi ya watu milioni moja katika mkoa wa Hassakeh ambao hapo awali walipata maji kutoka eneo la Alouk, sasa wanategemea maji yanayosukumwa kutoka umbali wa maili 12, sana na kilomita 20.

**JANGA LA MATETEMEKO**

Mapema mwaka huu, Umoja wa Mataifa kupitia vyombo vyake ikaripotiwa kuwa mwaka mmoja baada ya matetemeko makubwa ya ardhi yaliyokumba Uturuki na Syria, Umoja wa Mataifa ukatamka mamilioni ya manusura waliokumbwa na matetemeko hayo pamoja na wenyeji waliowapatia hifadhi inazidi kudorora.

Mashirika ya Umoja wa Mataifa likiwamo la kuhudumia wakimbizi - UNHCR na lile la afya, WHO ikatoa tathmini hiyo kupitia wasemaji wake jijini Geneva, Uswisi.

Shabia Mantoo, Msemaji wa UNHCR anafafanua: "Uturuki ni moja ya nchi zinazoongoza duniani kwa kuhifadhi wakimbizi, ilhali Syria nayo ambako mamilioni ya watu wamefurushwa makwao kutokana na janga la miaka 13 sasa hata kabla ya tetemeko, inakumbwa na janga kubwa la kiuchumi."

Akaongeza: "Nchini Syria takribani asilimia 90 ya watu ni mahohehahe, milioni 12.9 hawana uhakika wa kupata chakula ilihali milioni 7.2 ni wakimbizi wa ndani."

Matetemeko hayo ya ardhi yanatajwa yaliikumba eneo la mpakani mwa nchi mbili hizo, Februari mwaka 2023 na kusababisha vifo vya zaidi ya watu 50,000 nchini Uturuki na zaidi ya 5,000 Kaskazini-Magharibi mwa Syria na maelfu wengine walijeruhiwa.

Uharibifu huo unatajwa ulikuwa mkubwa, kwa maelfu ya majengo, yakiwamo ya miundombinu muhimu kama shule na hospitali yaliporomoka kutokana na ukubwa wa tetemeko.

"Uturuki inahifadhi wakimbizi milioni 3.4, na tetemeko la ardhi limeathiri eneo ambalo ni makazi ya wakimbizi milioni 1.75," akasema, Msemaji anawajibika na wakimbizi.

Ofisa huyo wa UNHCR, akataja kuwapo madhara ya matetemeko yako dhahiri kwa wakimbizi na wenyeji wao. Anaongeza kuwa, kutokana na ongezeko la mahitaji, wakimbizi wengi wakaamua kutumia mbinu mbadala za kuishi, ikiwemo kupunguza mlo na kukopa fedha zaidi.

"Janga hili tayari limekuwa na madhara kwenye afya ya akili na ustawi wa jamii husika. Watu wengi wamepoteza familia na marafiki," anasema Mantoo.

Kwa upande wa WHO, inaelezwa kuwa madhara ya tetemeko hilo yatadumu kwa miaka kadhaa ijayo ambapo watu wengi wataendelea kuishi kwenye makazi ya muda.

"Nchini Uturuki, tetemeko limesababisha uwepo wa mahitaji mapya na ya dharura ya kiafya kwenye jamii zilizoathiriwa, ikiwamo kwa wakimbizi na wenyeji," anasema Tarik Jasarevic, Msemaji wa WHO.

Anaongeza kuwa janga hilo lilivuruga namna ya kufikia huduma za afya kwa wahitaji kama vile wajawazito na watoto wachanga, pia huduma za chanjo, usimamizi wa magonjwa yasiyo ya kuambukiza kama vile kisukari, afya ya akili, na huduma kwa watu wenye ulemavu.

Kwa zaidi ya muongo mzima, Syria imekuwa ikikabiliwa na changamoto kubwa ikiwemo mzozo uliodumu muda mrefu, ukosefu wa utulivu kiuchumi, janga la afya kama vile Covid -19, kipindupindu na sasa tetemeko la mwaka jana la ardhi.

Kutoka ofisi ya Mjumbe Maalum wa Umoja wa Mataifa kwa Syria, OSE, Jenifer Fenton, anatamka: "Baada ya matetemeko ya ardhi tumeshuhudia kiwango cha chini kabisa cha uhasama na mwelekeo mpya wa kidiplomasia katika janga la Syria.

"Hata hivyo, haikuleta maendeleo halisi. Kwa kusikitisha, mwaka 2023 umeshuhudia kuibuka upya na kwa kiasi kikubwa kwa mapigano, na hivyo kufanya hali ya kibinadamu kuwa mbaya zaidi na ukosefu wa mchakato wa maana wa kisiasa."

• ***Kwa mujibu vyanzo tofauti***

## Wabunge viti maalum wanapoambiwa, uchaguzi mkuu 2025 waende jimboni

**INATOKA UK. 11**

Mwakilishi huyo anasema ni jambo jema kuwepo kwa kanuni nafasi za viti maalumu kuhudumu kwa muda wa vipindi viwili tu, ili kuwapisha wengine kupata uzoefu na kujengewa uwezo na wale ambao wameshahudumu vipindi viwili kwenda majimboni kugombea.

Anasema licha ya kwamba jimboni kuna changamoto nyingi ambapo kwa mwanamke zinaweza kumletea shida ikiwemo mfumo dume ambao unawarejesha nyuma wanawake kuingia majimboni kugombea.

Anautaja woga na kutojiamini, hivyo ni vyema kujiamini na kuondosha woga na wakiingia majimboni wana uwezo wa kushinda.

"Mimi sina wasiwasi na wanawake ikifika muda wa kugombea kwa ajili ya uchaguzi mkuu wa 2025 wanawake waje katika Jimbo la Fuoni kugombea kwa pamoja na atakayeshinda ataongoza jimbo lakini wanatakiwa wajipange kupambana na wanaume," anasema.

Mwanajuma Kassim Makame, viti maalum mkoa wa Kaskazini Unguja, anasema ugumu uliopo wa kugombea jimboni ni kupambana na wanaume lakini kwenye viti maalum unapambana na wanawake pekee.

Anasema pia changamoto nyingine ni gharama za kifedha kwa ajili ya kampeni ambapo jimboni ni gharama kubwa zaidi kuliko kwenye nafasi za viti maalum.

Mhadhiri wa Chuo Kikuu Zanzibar (ZU), Dk. Sikujua Omar, anasema kwa vipindi hivyo wanawake watakuwa wamepata ujasiri na uzoefu na fedha za kuwawezesha kusimama majimboni kugombea nafasi za uongozi na kushinda.

Anasema viti maalum humwandaa mwanamke kwenda kwenye siasa za ushindani na ushawishi kwa wananchi kutokana na kujifunza kutoka kwa wengine.

Dk. Mzuri Issa Mkurugenzi wa Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake (TAMWA) Zanzibar, anasema ushiriki wa wanawake katika uongozi ni hatua muhimu kuelekea usawa wa kijinsia katika uongozi na maendeleo ya kijamii.

Hata hivyo, anasema uwakilishi wa wanawake katika nafasi za uongozi ni mdogo, akitaja ukosefu wa fedha ni moja wapo ya changamoto kubwa inayokwamisha wanawake kufikia malengo ya kuwa kiongozi.

# Kampeni uchaguzi serikali za mitaa wanawake wachangiana fedha

## • Ni kuwezesha kinamama kufanya kampeni

**Na Sabato Kasika**

KAMPENI za uchaguzi wa serikali za mitaa, zinaanza kesho hadi Jumanne ijayo Novemba 26. Ni muda kwa wagombea wa vyama mbalimbali vya siasa kumwaga sera na kile walichotumwa na vyama vyao kukitangaza majukwaani.

Wakati kampeni zinaanza, wanawake 12 kutoka baadhi ya kata za Dar es Salaam, wamepata Sh. milioni 1.2 kwa ajili ya kuendeshea kampeni hizo zitakazodumu kwa wiki moja.

Wanawake hao wanawania ujumbe wa serikali za mitaa katika kata za Mzinga, Kivule na Kipunguni wakinufaika na fedha zilizochangwa na kinamama 70 ambao ni wajasiriamali wadogo.

Kila mmoja katika michango hiyo, alikuwa akitoa Shilingi 200 kila siku kwa miezi minne, kazi inayoratibiwa na Kituo cha Sauti ya Jamii Kipunguni kuwezesha wanawake kutoka vyama mbalimbali vya siasa wanaoshiriki uchaguzi kunufaika.

Mkurugenzi wa kituo hicho, Seleman Bishagazi, analiambia gazeti hilo kuwa wagombea 12, kila mmoja amepewa Sh.100,000 za kampeni ili angalau kuwapunguzia makali kwenye jukumu hilo.

Akifafanua jinsi michango hiyo ilivyoanza, anasema moja ya majukumu yao ni kuhamasisha wanawake wajitokeze kwa wingi kuingia katika uongozi kwa kuwa mchango wao unahitajika kubadilisha na kuboresha maisha na kufikia maendeleo.

"Lakini moja ya changamoto ambayo wamekuwa wakisema licha ya kwamba wanaonekana wana uwezo wa kuongoza, ni ukosefu wa fedha za kufanikisha kampeni," anasema Bishagazi.

Anatoa mfano kuwa mgombea anaweza kupitishwa na chama chake, akateuliwa kuwani uongozi na kwamba chama chake kinaweza kumwambia agharamie kampeni lakini hana fedha.

"Kwa ujumla fedha zinahitajika kwa vitu mbalimbali katika kampeni, lakini kinamama wengi wanakwama kutokana na ukosefu wa fedha. Baada ya kubaini hilo tukaanzisha mkakati huu," anasema.

Anafafanua kuwa waliamua kuuanzisha kuwezesha wanawake wenye nia ya kugombea kwa kushirikisha wajasiriamali wanawake ambao wamefanikisha fedha hizo.

Bishagazi anasema wanawake 12 waliowezeshwe na wajasiriamali wenzao ni kutoka vyama vya CCM na CHADEMA ambao tayari wamekabidhiwa kitita tayari kwa kampeni.

"Ninajua kiasi cha fedha walichopewa siyo kingi, lakini angalau kwa mwanzo huu, ujumbe wetu wa kutaka kuinua wanawake wengi ili waingie wengi katika ngazi za maamuzi umefanikiwa," anasema.



Mwenyekiti wa kituo hicho, Fatma Twalib (kulia), akimkabidhi fedha Mwanahamisi Kassim wa CCM. **PICHA ZOTE: SABATPO KASIKA**



Rehema Mfaume wa CHADEMA aliyenufaika na mchango huo.

### NENO LA WANUFAIKA

Rehema Mfaume anayewania ujumbe wa serikali ya mtaa Kivule kwa tiketi ya CHADEMA, anasema hatua ya baadhi ya wajasiriamali hao kuchanga Shilingi 200 kila mmoja ili kusaidia kinamama wagombea bila kujali vyama kinaonyesha mshikamano.

"Mara nyingi kumekuwa na dhana kwamba wanawake hawapendani, lakini kitendo hiki cha wauza mihogo ya kukaanga, miguu ya kuku na vitu vingine vidogo kutuchangia fedha za kampeni, kimeonyesha mshikamano ambao kinamama tunao," anasema Rehema.

Aidha, mara nyingi watu wamekuwa wakichangishana fedha kwa ajili ya harusi na sherehe mbalimbali, lakini kwa Kituo cha Sauti ya Jamii Kipunguni imekuwa ni kinyume kwa kuhamasisha fedha kwa maendeleo, anasema.

"Mkakati wa aina ufike Tanzania nzima ili katika uchaguzi mkuu, wanawake watakaojitokeza kuwania udiwani, ubunge na hata urais, wapigwe tafu kwa ajili ya kufanikisha kampeni," anasema.

> Kwa ujumla fedha zinahitajika kwa vitu mbalimbali katika kampeni, lakini kinamama wengi wanakwama kutokana na ukosefu wa fedha. Baada ya kubaini hilo tukaanzisha mkakati huu.

Mnufaika mwingine wa Sh. 100,000 Mwanahamisi Kassim kutoka Kata ya Mzinga anayewania ujumbe wa serikali mtaa kupitia CCM, anasema kilichofanywa na wanawake wajasiriamali ni cha kuigwa.

"Wanawake bado tunahitaji kuongezewa nguvu ili tuweze kuwa wengi katika uongozi ili tulingane na idadi ya wanaume. Hivyo, hiki ambacho kimeanzishwa na wenzetu si haba," anasema Mwanahamisi.

Mwanahamisi anasema kuna umuhimu mkubwa kumuunga mkono mwanamke katika uongozi, kwa maelezo kuwa naye ana nafasi yake kwa maendeleo jamii na taifa kwa ujumla.

Happy Mhagama naye amejitosa kuwania ujumbe wa serikali ya Mtaa wa Machimbo Kata ya Kipunguni kwa mara ya tatu kupitia CCM, anasema amevutiwa na mkakati wa wanawake wenzake kuchanga fedha hizo.

### UCHAGUZI 2019

Monica John Ofisa ni Habari wa Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP), anasema kwa mujibu wa takwimu za uchaguzi wa serikali za mitaa ya mwaka 2019 asilimia 2.1 ya wenyeviti wa vijiji wanawake.

Ofisa habari huyo amewahi kusema hayo katika mafunzo ya waandishi wa habari kutoka mikoa ya Mtwara, Lindi, Pwani na Dar es Salaam yalifanyika jijini Dar es Salaam, kwamba takwimu hizo haziridhishi katika kuzingatia usawa wa kijinsia.

Kutokana na hali hiyo, anawahimiza waandishi wa habari kuandika habari zenye mlengo wa kijinsi, hasa katika kuhamasisha ushiriki wa wanawake wajitokeze kuwania nafasi mbalimbali za uongozi.

"Kutokuwa na viongozi wanawake kuanzia ngazi za maamuzi na serikali za mitaa mambo mengi ya kijinsia yatakuwa yanasahaulika katika sera, mipango, bajeti na nyenzo mbalimbali ambazo zinasaidia kuleta maendeleo katika taifa letu," anasema Monica.

Anasema zipo changamoto mbalimbali ambazo wanawake zinawakabili katika michakato ya uchaguzi kuanzia kwenye kuchukua fomu hadi kwenda kwenye kampeni.

"Zamani kulikuwa na ile hali kwamba wanawake hawapendani au hawawezi akamchagua mwanamke mwenzao. Huo ni mtazamo potofu lakini kuna mahali wapo wanawake wanamwamini mwanamke mwenzao, kwa hiyo waandishi wa habari hampaswi kuchukua mtazamo hasi, badala yake mhamasishe mtazamo chanya ili wengine waamke," anasema.

# Faye, Sonko hawakamatiki, wapata ushindi wa kishindo

## • Kura za waliokubali, azma yao kuisuka upya nchi

**Na Mwandishi Wetu**

CHAMA tawala nchini Senegal cha PASTEF, kimejitangazia kupata ushindi wa kishindo katika uchaguzi wa bunge uliofanyika Jumapili iliyopita.

Ni chama kilichompinga rais wa zamani wa nchi hiyo, Macky Sall na kumtoa madarakani na kimekuwa na umaarufu mkubwa miongoni mwa vijana wa nchi hiyo.

Chama hicho kinaamini kuwa hatua hiyo ya ushindi ni ya kufungua njia kwa kutekeleza azma yake ya kuleta mabadiliko hasa vita dhidi ya rushwa na kutumia utajiri wa gesi na mafuta kuibadilisha kiuchumi nchi hiyo.

Vyombo vya habari nchini humo vinaripoti kwamba chama hicho kinasema kinaelekea kupata viti 119 hadi 131 katika bunge la viti 165 kwa mujibu wa makadirio ya matokeo ya awali yanayojulikana hadi sasa.

Taarifa za vyombo vya habari zinasema PASTEF imepata ushindi kwenye matokeo ya vituo vingi vya uchaguzi ambako imetangaza matokeo yao ya awali, kikivishinda vyama vikuu viwili vya upinzani.

Uchaguzi ulifanyika kwa amani nchi nzima ambako inaelezwa tayari asilimia 90 hadi 95 ya kura zimeshahesabiwa. Msemaji wa serikali Amadou Sarre, anawashukuru wapigakura kupitia kituo cha televisheni cha TFM akisema Wasenegali wamekipa ushindi mkubwa chama chake.

Rais Diomaye Faye, aliyeshinda uchaguzi wa rais Machi mwaka huu na kuahidi kuiletea Senegal mageuzi ya kiuchumi, kupambana na rushwa na kuleta mabadiliko katika masuala ya haki kwenye watu ndani ya jamii, anazidi kung'ara zaidi.

Ahadi hii ndiyo iliyowapa matumaini wananchi na hasa miongoni mwa idadi kubwa ya vijana wa taifa hilo la Afrika Magharibi wanaokabiliana na mfumuko wa bei, umasikini na ukosefu wa ajira.

Lakini, yote hayo alishindwa kuyatekeleza kutokana na bunge lililokuwa likiongozwa na upinzani kumzuia, hatua iliyomfanya Rais Faye kulivunja na kuitisha uchaguzi huu wa mapema wa bunge.

Karine Bouaye ni miongoni mwa wapiga kura aliyetoa maoni yake baada ya uchaguzi.

"Bunge lililopita la 14 halikutufurahisha. Pengine bunge hili la sasa litakuwa bora, likiwa lina watu watakaokuwa bora kwa taifa letu."

Vyanzo mbalimbali vimeeleza kwamba idadi ya waliojitokeza kupiga kura Jumapili ilikuwa ndogo ikilinganishwa na iliyoshiriki uchaguzi wa rais.



Rais wa Senegal Bassirou Diomaye Faye na Waziri Mkuu Ousmane Sonko . Wameshinda kwa kishindo uchaguzi wa wabunge. **PICHA: MTANDAO**

> Takriban Wasenegal milioni 7.3 walijiandikisha kupiga kura kuchagua watakaokalia viti 165 vya bunge la nchi hiyo kwa kipindi cha miaka mitano ijayo.



Mmoja wa wananchi wa Senegal akipiga kura.

Takriban Wasenegal milioni 7.3 walijiandikisha kupiga kura kuchagua watakaokalia viti 165 vya bunge la nchi hiyo kwa kipindi cha miaka mitano ijayo.

Rais wa zamani Makcy Sall, anaongoza chama cha upinzani cha TAKKU WALLU akiwa nje ya Senegal, na Jumapili iliyopita chama hicho kilidai kwamba uchaguzi ulikumbwa na udanganyifu na wizi mkubwa wa kura uliofanywa na chama tawala cha PASTEF, ingawa hakikutoa ufafanuzi wa madai yake.

Kufuatia hatua hiyo, Rais wa zamani Macky Sall, Waziri Mkuu Amadou Ba na Meya wa Jiji la Dakar mji mkuu wa nchi hiyo, Barthelemy Dias, ambao walikuwa wakiongoza muungano tofauti wa upinzani, wamekubali kushindwa.

Kupiga kura kulifanyika kwa amani kote nchini humo Jumapili iliyopita , ingawa kulikuwa na kukabiliana kwenye baadhi ya maeneo kati ya wafuasi wa vyama tofauti katika maandalizi ya uchaguzi huo.

Ushindi wa Diomaye Faye rais mdogo mwenye miaka 45 sasa kunarejesha kumbukumbu kwenye siasa za Senegal ambazo ziliwavutia watu wengi.

Alitupwa jela miezi kadhaa pamoja na mshirika na Ousmane Sonko, na waliachiwa huru wakati wa uchaguzi mkuu wa rais na wawili hao wakiachiliwa wiki moja kabla ya uchaguzi huo.

Kupambana na umaskini, dhuluma na ufisadi ni ajenda kuu ya Faye. Alipoingia madarakani Machi mwaka huu pamoja na Sonko ambao waliunda jopokazi la muungano ili kukabiliana na ufisadi.

Mambo mengine yanayopewa kipaumbele na gesi, mafuta, uvuvi na ulinzi lazima yote yajadiliwe upya ili kuwahudumia vyema watu wa Senegal, anasema Faye.

Faye alivunja ukimya, baada ya kupigiwa debe na Sonko hadi akawa rais kijana, alimteua mshauri na mtetezi wake huyo Ousmane Sonko kuwa Waziri Mkuu.

Itakumbukwa kuwa ni baada ya Sonko kuzuiliwa kuwania urais kutokana na mashtaka mbalimbali yaliyomchafua kijamii na kisiasa.

Wawili hao wanaahidi ajenda ya kubadilisha ushirikiano wa kisiasa na kiuchumi, kupitia upya mikataba ya mafuta , gesi na uvuvi na kuanzisha upya mamlaka ya Senegal, ambayo walidai imeuzwa.

Mapema mwaka huu, nchi hiyo ya Afrika Magharibi ilishuhudia ghasia mbaya katika miongo kadhaa kabla ya uchaguzi wa rais. Rais wa wakati huo Macky Sall, anadaiwa kuchelewesha kupiga kura kulikokuwa kumepangwa hapo awali mnamo Februari 2024.

Hali hiyo iliingiza nchi katika machafuko. Hatua hiyo ilisababisha maandamano mabaya, pamoja na kusukuma mahakama ya juu zaidi ya nchi kuingilia kati.

Baada ya mkwamo huo, uchaguzi hatimaye ulifanyika Machi 24, 2024 na kumpa ushindi mkubwa Faye mgombea asiyejulikana aliyeteuliwa na Sonko ambaye wakati huo alikuwa al maarufu. Lakini miezi saba tangu kupiga kura, ahadi hazijatimizwa, huku Sonko akililaumu bunge linaloongozwa na upinzani kwa kushindwa kupitisha sheria zinazohitajika kutekeleza mageuzi yaliyoahidiwa.

Tishio kubwa kwenye malengo ya chama cha PASTEF ni muungano usiotarajiwa wa vyama viwili vya upinzani, kikiwemo cha Alliance for the Republic (APR), kinachoongozwa na rais aliyeshindwa Macky Sall.

Kinyang'anyiro hicho pia kinajumuisha miungano miwili midogo ya upinzani mmoja ukiongozwa na Meya wa Dakar, Barthelemy Dias.

Mariam Wane Ly, mbunge wa zamani na mwanamke wa kwanza kuingia katika siasa za Senegal, anasema kampeni ya uchaguzi iliwapa viongozi nafasi ya kueleza ajenda zao na alitarajia PASTEF kuwashinda wengine.

**BBC/ALJAZEERA**



## Wazee waanza kukemea vitendo ukatili wa kijinsia

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

CHAMA cha Wazee Wastaafu Tanzania mkoani Dodoma kimeeleza namna kilivyojipanga kutekeleza wajibu wake kwa jamii ikiwamo kukemea vitendo vya ukatili wa kijinsia na mmomonyoko wa maadili.

Akizungumza jana jijini hapa baada ya kukabidhiwa ofisi, Katibu Mkuu wa chama hicho, George Andala, alisema kutokana na kuwapo na wimbi la ukatili wa kijinsia na mmomonyoko wa maadili wamejipanga kutoa elimu na kukemea jamii ili kukomesha hali hiyo.

Aidha, alisema watashirikiana na serikali kutoa elimu ya utunzaji wa mazingira kwenye maeneo ya hifadhi ya vyanzo vya maji ikiwamo eneo la Bonde la Mzakwe.

"Tunaishukuru ofisi ya mkuu wetu wa Wilaya ya Dodoma mjini kwa kutupatia ofisi na tunaahidi tutajipanga kuelimisha juu ya utunzaji wa mazingira hasa kwenye Bonde la Mzakwe, hii ni pamoja na ukemeaji wa vitendo vya kikatili na tabia za matumizi ya dawa ya kulevya na vitendo vya utoaji rushwa," alisema.

Makamu Mwenyekiti wa chama hicho, Rashidi Mamu, alisema kupatikana kwa ofisi hiyo hivi sasa kutawaondolea hali ya kutembea na mikoba yenye nyaraka zao mitaani.

Alisema kwa kipindi kirefu viongozi hao wamekuwa wakitembea na mikoba ikiwa na nyaraka kutokana na kukosa ofisi na kushindwa utoaji wa huduma za kijamii zinazohitaji busara zao.

Awali, Ofisa Tarafa wa Wilaya ya Dodoma, Zainab Issa, alisema kuwa anaamini ofisi hiyo itatumika kwa malengo husika katika kuwatatua kero zinazoikabili jamii.

Alisema kuwa serikali inatambua mchango mkubwa walioufanya wastaafu hao wakati wakifanya kazi, hivyo kwa busara zao hizo wanaamini ahadi walizoziahidi wataenda kuzitatua bila kujali itikadi ya aina yoyote na kutanguliza uzalendo.

Alisema: "Sisi kama serikali tumewatua mzigo wa kutembea na mabegi ambayo kuna nyaraka zenu muhimu, hivi sasa mtaziweka kwenye ofisi yenu hii, ni imani yetu tutayaona mabadiliko makubwa kutoka kwenu kutokana na ufanyaji kazi zetu".

# 'TAKUKURU rafiki' yafikia kata 21 Dodoma

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa nchini (TAKUKURU), mkoani Dodoma, kupitia programu ya 'Takukuru Rafiki' imetoa elimu na kutatua kero zenye viashiria vya rushwa kwenye kata 21 mkoani humo.

Akizungumza jana na waandishi wa habari, Mkuu wa TAKUKURU Mkoa wa Dodoma, Victor Swella, alisema programu hiyo ina lengo la kuisogeza jamii karibu na taasisi hiyo ili kutoa ushirikiano kwenye mapambano dhidi ya rushwa katika maeneo mbalimbali.

"Programu ya Takukuru rafiki inasaidia sana kuelimisha jamii juu ya madhara ya utoaji na upokeaji rushwa, jamii inazidi kupata uwelewa," alisema Swella.

Alifafanua kuwa katika utekelezaji wa programu hiyo wamekusanya kero 217, kati ya hizo baada ya uchambuzi uliofanywa na maofisa wa taasisi hiyo, kero 137 zimetatuliwa na wananchi kupatiwa mrejesho.

Mkuu huyo alisema kwenye utekelezaji wa jukumu la utoaji elimu kwa njia ya mikutano ya hadhara wamewafikia wananchi 21,282 na wanafunzi wa vyuo 24,086.

Alisema moja ya vipaumbele walivyojiwekea ni pamoja na kuhakikisha wanazuia vitendo vya rushwa katika maeneo mbalimbali ikiwamo maeneo ya kazi.

"Kipaumbele kingine ni kuongeza kasi ya kufanya uchunguzi za tuhuma zilizobainishwa katika taarifa ya Mkaguzi wa na Mdhibiti wa Hesabu za Serikali juu ya malalamiko ya matumizi mabaya ya ofisi na mamlaka katika idara ya ardhi kwenye jiji la Dodoma," alisema.

Alisema TAKUKURU itaendelea kuelimisha vijana kwa kushirikiana na Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora na Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya (DCEA).




Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Mkalama, mkoani Singida, James Mkwega (kulia), akizungumza na wadau wa uchaguzi wa serikali za mitaa kwenye mkutano uliowashirikisha viongozi wa vyama vya siasa, dini, madiwani, wazee mashuhuri, wasimamizi wasaidizi wa uchaguzi na watumishi wa serikali, wilayani humo, mwishoni mwa wiki. **PICHA: THOBIAS MWANAKATWE**

# Viongozi wa dini, wazee waombwa kuhamasisha ushiriki uchaguzi

**Na Thobias Mwanakatwe,** MKALAMA

VIONGOZI wa dini, wanasiasa na wazee maarufu katika Wilaya ya Mkalama, wameombwa kuhamasisha wananchi kujitokeza kushiriki katika Uchaguzi wa Serikali za Mitaa utakaofanyika Novemba 27, mwaka huu.

Mkurugenzi wa halmashauri hiyo ambaye pia ni Msimamizi wa Uchaguzi katika Wilaya ya Mkalama, Asia Messos, aliyasema hayo juzi kwenye mkutano wa wadau wa uchaguzi uliowashirikisha viongozi wa vyama vya siasa, viongozi wa dini, madiwani na wazee maarufu kutoka vijiji vyote vya wilaya hiyo.

Alisema ni muhimu viongozi hao wakahamasisha wananchi kushiriki katika uchaguzi huo muhimu kwao kwa kuwa wanakwenda kuchaguliwa viongozi ambao muda wote wanakuwa karibu nao.

"Nitoe rai kwa viongozi na wananchi kuwahimiza wananchi kushiriki uchaguzi ili wasipoteze haki yao ya msingi kwani ukipiga kura unakuwa na haki hata ya kumhoji kiongozi uliyempigia kura, lakini kama hujamchagua utashindwa sababu hujampigia kura," alisema.

Messos alisema katika halmashauri hiyo utafanyika uchaguzi wa kuchagua wenyeviti wa vijiji 70, wenyeviti wa vitongoji 388, wajumbe makundi mchanganyiko 732 na wajumbe wa Halmashauri ya Kijiji kundi la wanawake 560.

Hivyo, alitoa rai kwa vyama vya siasa wakati wa kampeni wasitumie lugha chafu kwa kuwa wananchi wanachohitaji ni kusikiliza sera na kufanya maamuzi ya kumchagua mgombea wa chama ambaye ana sera nzuri za kuwaletea maendeleo.

Nao washiriki wa mkutano huo walisema wananchi waachwe huru wachague viongozi wanaowataka, hivyo wasitishwe wala kushawishiwa na rushwa.

Shekhe wa Kata ya Ibada, Mussa Seleman Mussa, alisema iwapo wananchi wataachwa huru kuchagua viongozi wanaowataka bila kushawishiwa na rushwa watachaguliwa viongozi wazuri ambao wataweza kuwaletea maendeleo wananchi katika maeneo yao.

"Ukiwa na mgombea wako mfukoni ujue lazima utaharibu uchaguzi, serikali iweke mazingira mazuri wananchi wasipewe vitisho waache wachague viongozi wanaowataka wao," alisema.

Naye Mchungaji wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) Usharika wa Nkalakala, Emmanuel Nkulu, alisema wakati wa kampeni wagombea wazungumze sera za vyama vyao bila kutoa lugha chafu ambazo hazina maana.

"Wagombea msinunue wapigakura na ili uchaguzi uwe mzuri basi turuhusu mchanganyiko wa viongozi kwani kufanya hivi ndio kusaidia kuharakisha upatikanaji wa maendeleo ya haraka," alisema.



# Chunya yapata dawa kumaliza migogoro wakulima, wafugaji

**Na Nebart Msokwa,** CHUNYA

WILAYA ya Chunya mkoani Mbeya imekamilisha mchakato wa kuanzisha kongani tatu za malisho ya mifugo zenye ukubwa wa hekta zaidi ya 100,000 kwa lengo la kumaliza migogoro ya ardhi kati ya wafugaji na wakulima ambayo imekuwa ikiibuka mara kwa mara.

Maeneo yaliyotengwa yanatarajiwa kuwekewa miundombinu muhimu kwa ajili ya mifugo yakiwamo majosho, malisho ya kisasa na mabirika maalumu kwa ajili ya kunyweshea mifugo maji ili isitoke nje ya maeneo hayo.

Mkuu wa Wilaya ya Chunya, Mbarak Batenga, aliyesema hayo juzi kwenye mkutano na wafugaji wa Kata ya Sangambi ambao uliitishwa na Katibu Mkuu wa Chama cha Wafugaji Tanzania, Mathayo Daniel kwa lengo la kusikiliza kero za wafugaji.

Batenga alisema mchakato wa uanzishaji wa kongani hizo umekamilika katika ngazi za chini na sasa umewasilishwa katika Wizara ya Mifugo na Uvuvi kupata kibali na baraka za serikali kuu ili waendelee na ujenzi wa miundombinu.

Alisema uanzishwaji wa kongani hizo utakuwa ndiyo suluhisho la migogoro ya wafugaji na wakulima ambayo imekuwa ikisababisha machafuko katika maeneo mbalimbali kutokana na wafugaji kuchungia mifugo kwenye mashamba.

Alisisitiza kuwa wakishakamilisha uandaaji wa maeneo hayo kutakuwa na utaratibu maalumu wa wafugaji kupelekwa katika maeneo hayo ili kuepusha migogoro kuibuka wakati mwingine.

"Kuna baadhi ya wafugaji wamekuwa wakihama kutoka eneo moja kwenda lingine kwa ajili ya kutafuta malisho, watu hawa huwa siyo rafiki wa mazingira na pia wamekuwa wakivamia maeneo ya wakulima, tunataka tuweke mazingira haya rafiki kwa wafugaji wetu," alisema Batenga.

Hivyo, aliwataka wafugaji walioko ndani ya wilaya hiyo kuendelea kufuata sheria na taratibu zilizowekwa wakati serikali ikiendelea na mikakati ya kuwaboreshea mazingira ya mifugo yao.

Katibu Mkuu wa Chama cha Wafugaji Tanzania(CCWT), Mathayo aliipongeza serikali ya wilaya hiyo kwa kubuni wazo hilo kwa maelezo kuwa katika maeneo mengi nchini wafugaji hawathaminiwi na hivyo wamekuwa wakijiona kama wakimbizi.

Alisema wafugaji wamekuwa wakifukuzwa na serikali katika maeneo mbalimbali bila kutengewa maeneo mbadala ya kwenda kuchungia mifugo yao na hivyo kuwafanya baadhi yao kukata tamaa ya kuendelea na ufugaji.

"Tunakupongeza sana Mkuu wa Wilaya na timu yako kwa ubunifu mlionao, tunachoweza kuomba kwa sasa ni kuyalinda maeneo yote ambayo yametengwa na vijiji kwa ajili ya malisho ili yasivamiwe na kuzua migogoro mingine," alisema Mathayo.

Mwenyekiti wa Chama cha Wafugaji Wilaya ya Chunya, Shang'ai Ole Lapori alisema kutokana na wingi wa mifugo wilayani humo, kwa hali ya malisho siyo nzuri hasa kipindi cha kiangazi ambacho kunakuwa na ukame katika maeneo mengi.

Alisema baadhi ya wafugaji kutoka katika mikoa mingine nchini wamekuwa wakihamia kinyemela na mifugo yao ndani ya wilaya hiyo na hivyo kusababisha wakose takwimu sahihi za mifugo.




Mkuu wa Wilaya ya Songwe, Solomon Itunda, akisisitiza jambo kwa wachimbaji wadogo wa dhahabu, wakati wa uzinduzi wa mtambo wa kisasa wa kuchenjua madini hayo wa Kampuni ya Green Pacific Investment Ltd, wilayani humo juzi, ulionunuliwa kwa gharama ya Sh. bilioni 10 za mkopo uliotolewa na Benki ya NMB. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Serikali yapongeza wachimbaji wadogo kupewa mikopo

**Na Nebart Msokwa,** SONGWE

SERIKALI wilayani Songwe, imeipongeza Benki ya NMB kwa kuendelea kutoa mikopo yenye masharti nafuu kwa wachimbaji wadogo wa dhahabu wilayani humo kwa lengo la kuwasaidia kuboresha shughuli zao ikiwamo ununuzi wa mitambo ya kisasa.

Mkuu wa Wilaya ya Songwe, Solomon Itunda, aliyesema hayo juzi alipokuwa anazindua mtambo wa kisasa wa kuchakata madini wa Kampuni ya Green Pacific Investment LTD inayojishughulisha na uchimbaji wa madini katika Kijiji cha Maleza kilichopo Kata ya Mbangala wilayani humo.

Mtambo huo umenunuliwa na kampuni hiyo kwa gharama ya zaidi ya Sh. bilioni 10 ambazo kampuni hiyo imekopeshwa na Benki ya NMB ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa mikakati ya benki hiyo ya kuboresha sekta hiyo.

Itunda alisema benki hiyo imetekeleza moja ya malengo ya serikali ya kuwawezesha wananchi ambao wana nia ya kuwekeza kwenye shughuli mbalimbali za uzalishaji wakiwamo wachimbaji na wanaowekeza kwenye viwanda.

"Kwa niaba ya serikali nawashukuru sana benki ya NMB kwa kuwasaidia wachimbaji katika wilaya yetu, mtambo huu utasaidia kuboresha shughuli za wachimbaji wetu na nawashauri wachimbaji wengine mchangamkie fursa za mikopo hii ili muongeze uzalishaji," alisema Itunda.

Meneja wa NMB Tawi la Songwe, Yohana Bundala, alisema mkopo huo ni sehemu ya mikakati ya benki hiyo kuwasaidia wachimbaji wa madini nchini kuboresha shughuli zao na kuongeza uzalishaji ili kukuza uchumi wa wananchi na taifa.

Alisema mpaka sasa benki hiyo imewakopesha wachimbaji zaidi ya Sh. bilioni 70 ikiwamo kampuni hiyo ambayo imeamua kuboresha vitendea kazi.

Alisema mtambo huo ukikamilika utakuwa na uwezo wa kuchakata na kuchenjua tani 10 za mawe kwa saa tofauti na mitambo ya awali ambayo ilikuwa inachakata tani tatu kwa saa na kwamba mtambo huo utaongeza hata ubora wa dhahabu.

Hata hivyo alisema benki hiyo imeanzisha kitengo maalumu kilichojikita katika kushughulikia masuala ya madini katika idara ambazo zinashughulikia wachimbaji wadogo na wakubwa.

Mkurugenzi wa Kampuni ya Green Pacific LTD, Fredric Meshack, aliishukuru NMB kwa kumpatia mkopo huo akidai kuwa utasaidia kuongeza uzalishaji na hata kufundishia wachimbaji wengine wadogo.

# Wananchi watakiwa kushiriki kampeni za vyama

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

MSIMAMIZI wa Uchaguzi wa Serikali za Mitaa katika Halmashauri ya Mji wa Njombe, Kuruthum Sadick, amewataka wananchi kujitokeza katika kampeni za vyama vya siasa zinazoanza Novemba 20 hadi 26 ili kusikiliza sera zitakazowasaidia kuchagua viongozi sahihi.

Kuruthum alitoa kauli hiyo jana wakati akizungumza na waandishi wa habari katika ukumbi wa halmashauri hiyo ambapo alisema muda wa kampeni ni kuanzia saa mbili asubuhi hadi saa 12 jioni.

Alisema wananchi wanapaswa kujitokeza kwa wingi katika kampeni hizo ili waweze kuchagua viongozi sahihi kwa kuwa tayari wagombea wameshawasilisha ratiba zao za kampeni.

"Kwa hiyo mimi nitaomba kwa vyama vyote Chama Cha Mapinduzi (CCM) na Chama cha Demokrasia na Maendeleo CHADEMA, niombe waweze kufuata utaratibu wa ratiba ambayo walijiwekea ili kuweza kufanya kampeni zao kwa amani," alisema Kuruthum.

Aidha, alitoa wito kwa wananchi mjini humo walioji-andikisha kwenye daftari la mkazi kwamba wajitokeze kwa wingi siku ya kupiga kura na kuchagua viongozi watakaoongoza katika mitaa, vijiji na vitingoji.

Alisema kwa upande wa makundi maalumu, halmashauri imejipanga kuweka mazingira rafiki ili kila mtu apate nafasi ya kupiga kura bila kikwazo chochote.

"Wananchi wale ambao wanamahitaji maalumu, kinamama, wazee na walemavu tumeweza kujipanga kwamba watapewa kipaumbele kwa kuwawekea mazingira rafiki kwa wote," alisema Kuruthum.

Alisema kwa halmashauri hiyo ni vyama vya siasa viwili pekee ambavyo ni CCM na CHADEMA ndiyo vilivyosimamisha wagombea.

Mmoja wa wananchi mjini hapa, Mary Mligo, alisema wamejiandaa vizuri kupiga kura licha ya wachache kuona kwamba suala hilo halina umuhimu.

"Niwaombe wananchi wenzangu tuanzie kwenye kampeni tukasikilize ili siku ya kupiga kura tukachague viongozi sahihi na tuachane na malalamiko muda sahihi ndiyo sasa," alisema Mary.

Alisema kushiriki kwenye Uchaguzi wa Serikali za Mitaa ni jambo la muhimu, hivyo wanapaswa kujitokeza katika hatua zote ikiwamo kushiriki kwenye kampeni.





## Uhusiano Tanzania, Hispania wakuza afya ya jamii

**Na Mwandishi Wetu**

MAKAMU wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Othman Masoud Othman, amesema uhusiano wa asili kati ya Tanzania na Hispania umeongeza fursa nyingi za maendeleo ikiwemo kukuza afya ya jamii.

Aliyasema hayo juzi wakati akizungumza na madaktari bingwa na wataalamu, alipotembelea Hospitali ya 'De Clinica CEMTRO', Mjini Madrid, Nchini Hispania.

Alisema uhusiano huo wa tangu asili unahitaji kuendelezwa kwa lengo la kusaidia uimarishaji wa kutoa huduma bora za jamii, ili kufanikisha adhma ya kujiletea maendeleo ya kweli.

Alisema kuwa adhma ya kuwaleta madaktari bingwa kuja nchini, kwa lengo la kuimarisha afya ya jamii na huduma za upasuaji itatekelezwa kama ambavyo imeahidiwa kupitia ziara hiyo.

Alisema Serikali ya Zanzibar imepokea vyema ahadi ya msaada wa vifaa tiba na madaktari bingwa wakiwemo wa mifupa, magonjwa ya watoto na kinamama, ambao wameahidi kuja Tanzania kwa lengo la kuwaongezea ujuzi wataalamu wa afya.

Mwanzilishi wa Hospitali ya De Clinica CEMTRO, Profesa Pedro Guillén García, alisema ili kuijengea ubora taaluma ya afya duniani ni vyema kukuza ushirikiano na ujuzi kwa wale waliobobea zaidi katika fani mbalimbali.

Alisema vilevile kwa madaktari wengine wenye hari, hasa wasiokuwa na nyenzo za kutosha kutoka mataifa yanayoendelea.

Prof. Pedro alisema kwa upande wa taasisi yao hiyo, ambayo ni tegemeo nchini Hispania, hawana budi kutekeleza ombi la Serikali ya Zanzibar la kuwaleta madaktari bingwa kuja kuikuza sekta ya afya Zanzibar.

Mmoja wa madaktari kutoka hospitali hiyo, Dk. Isabel Pedro Guilen alisema wamezunguka mataifa mengi duniani kwa ajili ya kutoa huduma, kwamba kwa sasa wanajiandaa kuifikia Tanzania.

# RC aeleza mchango wa Samia, Mwinyi kuwainua wajasiriamali

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MKUU wa Mkoa wa Kaskazini Unguja, Rashid Hadid Rashid, amesema mchango wa Rais Samia Suluhu Hassan na Dk. Hussein Ali Mwinyi ni mkubwa katika kuwainua na kuwawezesha wajasiriamali katika kuwapatia mikopo.

Aliyasema hayo jana Mahonda Mkoa wa Kaskazini Unguja wakati akifungua mkutano uliowashirikisha wajasiriamali wa mkoa huo wakati wa kupewa elimu kuhusu programu ya imarisha uchumi na mama Samia.

Alisema hatua hiyo imesiadia wananchi katika kukuza uchumi wao kupitia sekta mbalimbali ikiwemo kilimo ambapo wananchi wa mkoa huo shughuli yao kubwa ni kilimo.

Alisema maeneo ya kilimo haswa yanayofanywa na wanawake yamepelekwa umeme kwa ajili ya kulima kilimo cha kisasa chenye tija na kuwapatia kipato.

Mahonda alisema wananchi wanahitajji nguvu za ziada katika kuimarisha uchumi wa bluu katika mkoa huo licha ya serikali kuwawezesha wavuvi kwa kutoa boti 270 ili kuondokana na umaskini.

Alisema kuhusu biashara ndogo wananchi wa mkoa huo hasa wanawake wamejikita huko lakini wanahitaji kuwezeshwa ili kuendeleza biashara zao.

Alisema wanawake ndio walezi wa watoto lazima uchumi wao uimarishwe ili kuzihudumia familia vizuri na kuondokana na umaskini.

"Tukiimarisha shughuli za kilimo na biashara zengine ndogo wananchi watanufaika hasa ikizingatiwa kuwa mkoa huo una hoteli zaidi ya 30 zenye hadhi tofauti, hivyo ni vyema kuitumia fursa hiyo vizuri" alisema.

Mshauri wa Rais wa masuala ya wanawake na makundi maalum, Sophia Mgema, alisema lengo la kutoa elimu hiyo ni kuyafufua majukwaa ya kuwezesha wananchi kiuchmi.

Alisema jukwaa hilo lina fursa nyingi ikiwemo kwenye kilimo, uvuvi, mama lishe, wakulima wa mwani na wafanyabiashara wadogo ili kupata maendeleo na uchumi kuimarika.

Katibu Mtendaji Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi (NEEC), Beng'i Issa, alisema IMASA imejielekeza katika makundi ya wanawake, vijana, wazee na watu wenye ulemavu na Rais Samia amepania kuyawezesha makundi hayo kwa kuyasaidia kiuchumi.

Alisema programu hiyo ya IMASA inaibua vipaumbele vya shughuli za wananchi wanazozifanya na kutolea mfano Mkoa wa Kaskazini kipaumbele kikubwa ni uvivi na utalii, hivyo ni vyema kuwa na mnyororo wa thamani wa kusaidia katika utalii na kilimo.

Mkurugenzi wa Wakala wa Uwezeshaji Zanzibar (ZEA), Juma Burhan alisema ZEA ipo mstari wa mbele kuwawezesha wananchi kiuchumi na kuwapatia mikopo.



Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi akiongozana na Mkewe, Mama Mariam Mwinyi akiagana na Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdalla (kulia), kabla ya kuondoka katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Abeid Amani Karume Zanzibar jana, kuelekea jijini Harare, nchini Zimbabwe kumwakilisha Rais Dk. Samia Suluhu Hassan katika Mkutano wa Dharura wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC), utakaofanyika leo. **PICHA: IKULU**

# Waziri ahimiza matumizi bora barabara kuepusha ajali

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

NAIBU Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi, Nadir Abdul- latiif Yussuf amewataka wananchi na madereva kutumia vyema barabara zinazojengwa kuepusha ajali za barabarani.

Alisema hayo Kikwajuni visiwani humo wakati akifungua kongamano la kujadili changamoto za ajali za barabarani Zanzabar.

Alisema takwimu zinaonyesha ongezeko kubwa la ajali za barabarani kwa miaka ya hivi karibuni kutofautisha na kipindi cha miaka ya nyuma.

Hivyo, aliwataka wananchi kuwaripoti madereva wanaosababisha ajali kwa kuchukua namba zao na kuzifikisha katika mamlaka husika.

Pia, alitumia nafasi hiyo kuzitaka taasisi zote zinazohusika na usalama barabarani kushirikiana kwa pamoja kuondosha tatizo la ajali za barabarani.

Vilevile, alilitaka Jeshi la Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani kuwaripoti madereva wote wanaohusika na ajali pamoja na kuwapa adhabu stahiki.

"Maredeva wamekuwa waendelea kusababisha vifo kwa kuwa adhabu wanazopewa ndogo, haziendeni na makosa ya usalama barabarani hivyo niliombe Jeshi la Polisi kutoa adhabu stahiki kwa madereva wote wanaosababisha ajali," alisema.

Katibu Tawala Mkoa wa Mjini Magharibi Unguja, Mohamed Ali Abdalla alisema ajali za usalama barabarani zimekuwa zikiongezeka kwa mwaka kwa asilimia 55 ambapo asilimia 18 ni Mkoa wa Kaskazini Ungua ambao unayoongoza.

Naye Ofisa Takwimu kutoka Kitengo cha Takwimu Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali, Ahmada Hassan Suleiman, alisema kwa kipindi cha mwaka 2020 - 2023, ajali 880 ziliripotiwa.

Alisema Wilaya ya Magharibi 'A' iliripotiwa ajali 160 sawa na asilimia 18.2, Wilaya ya Micheweni iliripotiwa kuwa na idadi ndogo ya ajali 29.

Alisema kuwa waathirika wengi waliripotiwa mwaka 2020 ambao kulikuwa na kesi 552, waliojeruhiwa ni 1,088 waliofariki ni 616 kwa kipindi cha miaka minne.

Alitumia nafasi hiyo kueleza kuwa idadi ya waathirika wa ajali za barabarani abiria 660 sawa na asilimia 38.7 ya waathirika wote walioripotiwa.

Sambamba na hayo alisema waliojeruhiwa wengi walikuwa ni abiria ambao ni 568 sawa na asilimia 62.6 ya waathirika wote na waliofariki dunia wengi walikuwa wapanda baskeli na pikipiki 302 sawa na asilimia 49.0.

Alisema idadi ya makosa ya barabarani 99,575 yaliripotiwa kwa mwaka ambapo makosa 99,370 yaliripotiwa kufanywa na wanaume na 205 wanawake.

Mkuu wa Jumuiya ya Magari ya Abiria Unguja, Khamis Mussa Khamis alisema matatizo ya ajali za barabarani yanasababishwa na madereva kutozingatia sheria za usalama barabarani.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA CHETI



**LIGHTNESS TUMSIFU KAWICHE** anatangaza kupotea kwa cheti cha kuhitimu kidato cha nne chenye Index No. **S0107/0016** Kilichotelewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **LUTHERAN JUNIOR SEMINARY SECONDARY SCHOOL** mwaka 2016, Cheti hiki kimepotea Jijini DAR ES SALAAM. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya Polisi: **PHQ/DAR/KIG/196219/2023**

## KUPOTEA KWA HATI YA KUSAFIRIA




**JOHN BARRY SANG'WA** anatangaza kupotelewa na hati yake ya kusafiria yenye namba TAE 389649 .Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/DAR/TEM/254622/2024.**

## KUPOTEA KWA CHETI



**TATU ALLI HAMISI** anatangaza kupotea kwa cheti cha kuhitimu darasa la saba chenye Index No. **PS 2004079-028** Kilichotelewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **NKUMBA PRIMARY SCHOOL** mwaka 2019, Cheti hiki kimepotea Jijini DAR ES SALAAM. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya Polisi: **PHQ/DAR/ILA/250497/2024**

## KUPOTEA KWA HATI YA KUSAFIRIA



**ERICK JOHOLA JOHOLA** anatangaza kupotelewa na hati yake ya kusafiria yenye namba **TAE 416545.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/SHI/KAH/1849/2024.**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**ALLY SALUMU MJUNGU,** Anatangaza kupotelewa na kadi ya Pikipiki aina ya **Boxer** yenye namba za usajili **MC907BUX,** CHASSIS NO **MD2A21BY3HWG87245,** ENGINE NO **PFZWHG77894.** Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo cha Polisi. TAARIFA YA POLISI: **PHQ/DOD/DOD/53083/2024**

---

**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA**
**WILAYA YA KINONDONI**
**MWANANYAMALA**
**SHAURI LA MADAI NAMBARI 247 LA 2024**
**OSMAN ABDULKADIR SADIK......MUOMBAJI**
**DHIDI YA**

- **LUZANE INVESTMENT LTD**
- **SAMAITA INVESTMENT PARTNERS LTD ....WADAIWA**

**WITO KUITWA SHAURINI**

- **LUZANE INVESTMENT LTD**
- **SAMAITA INVESTMENT PARTNERS LTD**

**POPOTE ULIPO/WALIPO;**
**OSMAN ABDULKADIR SADIK** Amefungua shauri mbele ya Baraza la Ardhi na Nyumba lililopo Kinondoni (Mwananyamala) Shauri husika limepangwa kutajwa tarehe 21 mwezi Novemba mwaka 2024 saa 03:00 Asubuhi mbele ya Mh. J.W. SILLAS Hivyo unahimizwa kuhudhuria mbele ya Baraza siku hiyo bila kukosa.

Imetolewa na kutiwa Saini na Mhuri wa Baraza hili leo tarehe 18 mwezi 10 mwaka 2024

MWENYEKITI

---

**IN THE DISTRICT COURT OF KOROGWE**
**AT KOROGWE**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO. 28098 OF 2024**
**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE CHRISPINUS ANDREA CHAMOTO**
**AND**
**IN THE MATTER OF THE APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION BY PIENSIA JOSEPH CHUWA**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 of probate Rules GN 369 OF 1963)**

All Person Claiming to have any interest in the Estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named petitioner.

Objections to the grant should be field on or before the 10th day of December 2024

Dated at Korogwe this 15th day of November 2024

RESIDENT MAGISTRATE
KOROGWE

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya KILOMBERO**

**Kituo cha KILOMBERO Mkoa ......................................**

**Jina la Mdai: SALEHE HAMISI KISIMA**

**Jina la Mdaiwa: HADIJA ALLY MSINGWA**

**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**(Kanuni ya 18 ya Kanuni za Utaratibu wa Madai katika Mahakama za Mwazo)**

**Kwa HADIJA ALLY MSINGWA**

**Kwakuwa mdai/wadai ameleta madai yake/yao kwamba (eleza hapa Habari za madai)**

**SHAURI LA MADAI YA TARAKA**

Hivyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii siku ya JUMATANO tarehe 13 Mwezi 11 Mwaka 2024 saa 5;00 Asubuhi kwa mujibu wa madai hayo na Kwakuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta shahidi/mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea.

**ANGALIZO:** Kama hautohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikathibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini, Mahakama inaweza kusikilizwa shauri bila ya wewe kuwepo. Hati hii imetolewa kwa amri na Muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 6 Mwezi 11 Mwaka 2024

HAKIMU
MAHAKAMA YA MWANZO KILOMBERO

---

**Magistrates Court (Approved Forms for the Primary Court**

**GN.NO 943 (Contd.)** **FOMU MIRATHI-3**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika Mahakama ya Mwanzo Wilaya ya Moshi**

**Kituo cha Moshi Mjini Mkoa Kilimanjaro.**

**Usimamizi wa mirathi Na 207/ 2024.**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU Mohamed Salim Mamuya wa Moshi Mjini.**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUWA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA Ally Mohamed Mamuya**

**TANGAZO**
**(Kanuni ya 5(2) ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote /maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu ,wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 28 Mwezi 11 Mwaka 2024 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

**Zingatia**
Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa
Wosia wa marehemu huyo upo mahakamani na waweza kukaguliwa.
Marehemu hakuacha wosia.
Futa isiyohusika
**Imetolewa leo tarehe 14 Mwezi 11 Mwaka 2024**

HAKIMU

---

**OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042,**
**DAR ES SALAAM.**
**MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail:**
**advertise@guardian.co.tz,**
**website:**
**www.ippmedia.com**

***Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi***

***Kwa Bei Poa***

***Tupigie: +255 - 0677 020701***

KWA MAHITAJI YA KUTANGAZA SUMMONS, KUPOTEA KWA CHETI, KUPOTEA KWA KADI YA GARI/PIKIPIKI NA USIMAMIZI WA MIRATHI.

TUPIGIE: +255 - 0677 020701 AU TEMBELEA OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,

PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.

E-MAIL: ADVERTISE@GUARDIAN.CO.TZ

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji
THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## Maaskofu Kenya wakataa mchango wa Rais Ruto

**NAIROBI,** Kenya

MAASKOFU wa Kanisa Katoliki Kenya, wamekataa dola 15,000, mchango uliotolewa na Rais Wiliam Ruto, wakisema kanisa halipokei michango ya kisiasa.

Aidha, walisema kukataa kunazingatia sera ya Baraza la Maaskofu la Kenya (KCCB) kuhusu michango ya kisiasa makanisani.




Taarifa ya KCCB, ilisema kukataliwa kwa michango kadhaa iliyotolewa katika Kanisa la Soweto, ni kutokana na maagizo ya KCCB.

Rais William Ruto alichangia dola 15,504 sawa na shilingi za Kenya milioni mbili katika ujenzi wa Nyumba ya Padri.

Pia alitoa ahadi ya shilingi milioni tatu kwa ajili ya ujenzi wa ziada na ununuzi wa mabasi ya parokia.

KCCB, katika taarifa yake hiyo na kusomwa katika makanisa yote ndani ya Jimbo Kuu Jumapili iliyopita, ilisisitiza umuhimu wa kuhifadhi uhuru na utakatifu wa Kanisa, pamoja na masuala ya kimaadili yanayozunguka michango ya kisiasa.

Akizungumza kwa niaba ya Jimbo kuu la Nairobi, Askofu mkuu Philip A. Anyolo, alisisitiza umuhimu wa majukwaa ya kanisa kutotumiwa na watu kujinufaisha kisiasa. **BBC**



Askofu Mkuu wa Metropolitan, Philip Anyolo akizungumza na waandishi wa habari.

# Russia kuijibu vikali Marekani, timu ya Trump yampinga Biden

**MOSCOW,** Marekani

BAADA ya Rais wa Marekani, kuiruhusu Ukraine kutumia makombora ya masafa marefu yaliyotengenezwa na nchi hiyo, hali ya wasiwasi imetanda duniani kutokana na majibu makali kutoka kwa kiongozi wa Russia, Vladimir Putin.

Katika jibu lililoonekana kuwa ni kali zaidi, Rais Putin alisema kombora lolote la Marekani litakalotua nchini mwake na kusababisha madhara kwa watu na mali zao litajibiwa kwa ukali unaofaa.

Taarifa kutoka Wizara ya Mambo ya Nje ya Russia, ilisema matumizi ya makombora ya masafa marefu ya Marekani dhidi ya nchi hiyo kutoka Ukraine yatasababisha majibu yafaayo na yanayoonekana.

"Shambulio kama hilo ndani ya ardhi ya Russia litawakilisha ushiriki wa moja kwa moja wa Marekani na satelaiti zake katika uhasama dhidi ya taifa letu," ilisema taarifa hiyo.

Rais Joe Biden aliidhinisha matumizi ya makombora kushambulia shabaha ndani ya Russia katika mabadiliko makubwa ya sera ya Marekani, miezi miwili kabla ya kuondoka katika Ikulu ya Marekani.

Haijafahamika iwapo hatua hiyo alishauriana na mrithi wake, Donald Trump, ambaye aliahidi kumaliza vita vya Russia na Ukraine.

Ukraine imekuwa ikitumia makombora ya Marekani yenye uwezo wa kufika hadi kilomita 300 sawa na maili 190.

Makombora mengine kutoka Ufaransa na Uingereza ya Storm Shadow ya masafa marefu, Ukraine imezuiwa kuyatumia kushambulia ndani ya Russia.

Uamuzi wa Biden wa kuondoa kikwazo hicho kwa upande wa Marekani, umekuja wakati ambao vita hivyo vinaingia siku yake ya 1,000 jana.

Vita hivyo vilianza Februari 22, 2022 wakati Russia ilipoivamia Ukraine na kuchukua majimbo ya Mashariki.

Katika hatua nyingine, uamuzi huo wa Rais Biden umeibua sintofahamu kwa timu ya Rais mteule wa Marekani, Donald Trump, wakieleza wazi kuwa hatua hiyo sawa na kuanzisha vita ya tatu ya Dunia.

Hata hivyo, Trump mwenyewe hajazungumza lolote, lakini msimamo wake unafahamika kuwa hataki kushiriki vita vya nje ya taifa hilo.

Rais Biden licha ya kuruhusu matumizi ya makombora hayo ya masafa marefu, ametoa mabilioni ya dola kuisaidia Ukraine.

Mtoto wa Trump, Donald Trump Jr alituma ujumbe kwenye ukurasa wake wa X, akieleza kwamba rais anajaribu kuanzisha Vita vya Tatu vya Dunia, kabla ya baba yake hajachukua madaraka.

Mfuasi mwingine wa Trump, Taylor Greene, alilaani hatua hiyo ya Biden, alisema wamarekani hawataki kufadhili au kupigana vita vya kigeni.

"Watu wa Marekani waliamua Novemba 5 dhidi ya maamuzi haya ya mwisho ya Marekani na hawataki kufadhili au kupigana vita vya kigeni. Tunataka kurekebisha shida zetu wenyewe," aliandika kwenye ukurasa wake wa X.

Uamuzi wa Biden haujathibitishwa rasmi na huenda usithibitishwe.

**Wakati huo huo**, Rais wa Ukraine, Volodymyr Zelensky alisema tangazo la vitisho lililotolewa na Russia halitobadilisha kitu, badala yake makombora yatazungumza yenyewe.

"Ukraine haitasalimu amri kwa wavamizi, na jeshi la Russia, litaadhibiwa kwa kukiuka sheria za kimataifa," Wizara ya Mambo ya Nje ya Ukraine, ilisema jana.

Hata hivyo, Zelensky alitarajiwa kuhutubia kikao maalumu cha Bunge la Ulaya wakati nchi hiyo ikiadhimisha siku hiyo muhimu.

Hatua hiyo inakuja wakati watu wanane, akiwemo mtoto, waliuawa katika shambulio la ndege isiyo na rubani kwenye eneo la kaskazini-mashariki mwa Ukraine la Sumy.

Jeshi la polisi la Ukraine, lilieleza ndege zisizo na rubani zilishambulia jengo la makazi katika mji mdogo wa Hlukhiv na kujeruhi watu 12 wakiwemo watoto wawili.

Katika ujumbe wake, Rais Zelensky alisema jengo hilo lilikuwa bweni la shule moja ya mtaani.

"Russia inaendelea kutisha mikoa yetu ya mpaka," Zelensky aliandika.

Katika video iliyosambazwa na rais, walionekana wafanyakazi wa dharura wakionekana wakipekua vifusi walipokuwa wakiendelea kutafuta waathiriwa. **BBC**



Rais wa Ufaransa, Emmanuel Macron akizungumza na Rais wa Marekani, Joe Biden wakati wa kikao cha kwanza cha Mkutano wa G20 2024 unaofanyika Brazil. **PICHA: GETTY IMAGES**

# Upinzani washinda Somaliland

**HARGEISA,** Somaliland

KIONGOZI wa upinzani katika jimbo la Somaliland, Abdirahman Cirro ameshinda katika uchaguzi wa rais uliofanyika wiki iliyopita.

Kwa mujibu wa Tume ya Uchaguzi ya Somaliland,Cirro ameshinda katika uchaguzi wa rais uliofanyika wiki iliyopita. Matokeo hayo ni kwa mujibu wa kituo cha habari cha mtandaoni cha Garowe ambacho, kimeinukuu tume hiyo.

Tume hiyo ilisema kiongozi huyo wa upinzani wa chama cha Waddani alipata asilimia 64 ya kura zote dhidi ya rais aliyeko madarakani Muse Bihi Abdi aliyepata asilimia 35.

Somaliland ni jimbo lenye utawala wake wa ndani baada ya kujitenga na Somalia tangu mwaka 1991,japo haijatambuliwa na nchi yoyote. **DW**

## HABARI MICHEZO

# FOUNTAIN GATE KUSAJILI MABEKI DIRISHA DOGO

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Fountain Gate imesema itaingia sokoni kipindi cha dirisha dogo la usajili linalotarajiwa kufunguliwa Desemba 15, mwaka huu, ili kusajili wachezaji wanaocheza safu ya ulinzi eneo ambalo limeonekana kupwaya ndani ya kikosi hicho.

Rais wa klabu hiyo, Japhet Makau, alisema hayo jana akitoa tathmini ya mwenendo wa timu yake katika michezo ya Ligi Kuu Tanzania Bara ambayo imecheza mpaka sasa.

Makau, amesema licha ya mwanzo mzuri wa timu yake, bado inakabiliwa na changamoto katika safu yake ya ulinzi ambayo inahitaji kufanyiwa maboresho.

**"Tumeangalia kiwango cha timu yetu kubwa ya wanaume, kwa kweli tumeridhika mpaka sasa tukiwa tunashika nafasi ya tano ya msimamo wa ligi katika michezo 11 tuliyocheza, tukiwa na pointi 17, ni mwanzo mzuri," alisema.**

Alisema pamoja na kuwa timu yake ina uwezo mkubwa wa kufunga mabao, lakini imekuwa ikiruhusu mabao mengi, hivyo wanataka kuimarisha ukuta wao.

"Hata hivyo, inaonekana kuwa tuna uwezo mkubwa wa kufunga mabao, ukiondoa mechi dhidi ya Simba ambayo tulifungwa mabao 4-0 hatukufunga bao, inawezekana kuwa ni timu moja kati ya timu mbili ambazo zimefunga mabao mawili katika kila mchezo, lakini tuna changamoto upande wa nyuma kwenye ulinzi, tumeruhusu mabao mengi, ni eneo ambalo tunalichukulia hatua katika kipindi cha dirisha dogo la usajili kuweza kufanya marekebisho kidogo eneo hilo ili kuhakikisha tunafanya vizuri, malengo yetu ni kumaliza ndani ya nafasi nne za juu kwenye Ligi Kuu," alisema.

Timu hiyo inayoshika nafasi ya tano kwenye msimamo wa Ligi Kuu ikicheza mechi 11 na pointi zake 17, imeshinda michezo mitano, sare mbili na kupoteza mechi nne.

Inashika nafasi ya pili kwa kufunga mabao mengi baada ya Simba yenye mabao 21, ikifunga mabao 20, lakini ikiruhusu pia mabao 20, ikiwa ni timu inayoongoza kwa kuruhusu mabao mengi, idadi sawa na KenGold inayoburuza mkia.

# *Prisons yaiendea gym JKT*

**Na Adam Fungamwango**

KIKOSI cha Tanzania Prisons kimepelekwa 'gym' kwa ajili ya utimamu wa mwili ili kujiandaa na mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya maafande wenzao JKT Tanzania Jumapili ijayo, mchezo utakaopigwa Uwanja wa Jenerali Isamuhyo uliopo Mbweni, Dar es Salaam, huku ikihitaji mechi moja ya kirafiki.

Kocha Mkuu wa timu hiyo, Mbwana Makata, amesema jana kuwa, ingawa wamekuwa wakiingia 'gym', mara mbili kwa wiki, lakini kwa sasa wameongeza dozi kwa sababu wanakwenda kucheza na timu ya maafande ambayo ina wachezaji wenye fikizi.

"Lazima tuongeze dozi, wachezaji wakiwa na fiziki sawa sawa watakuwa na pumzi, spidi na kuweza kufanya kila unachowaelekeza," alisema kocha huyo.

Alisema maandalizi wanayofanya kwa sasa ni makubwa kwani wanataka kushinda mchezo wa kwanza baada ya kutokea kwenye mapumziko ya Kalenda ya FIFA.

Pamoja na kwamba timu hizo zina pointi 10 kila moja, lakini JKT Tanzania ipo juu kutokana na uwiano mzuri na mabao ya kufunga na kufungwa ikiwa nafasi ya 11, huku Prisons ikiwa nafasi ya 12.

JKT Tanzania itakuwa ikicheza mchezo wake wa kwanza tangu mwezi uliopita wakati mechi zake zilipoahirishwa kutokana na basi lao kupata ajali jijini Dar es Salaam lilipokuwa likitoka jijini Dodoma kucheza dhidi ya Dodoma Jiji.




Kocha Mkuu wa Yanga, Sead Ramovic, akiongoza mazoezi ya timu hiyo jana katika viwanja vya Avic Town, Kigamboni, Dar es Salaam, pembeni ni winga Maxi Mpia Nzengeli. **PICHA: YANGA**

# Msigwa kupokea taarifa mchezo wa bao kutambuliwa rasmi duniani

**Na Mwandishi Wetu**

KATIBU Mkuu wa Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo, Gerson Msigwa (pichani chini), Jumamosi ijayo anatarajiwa kufungua kikao cha kupokea taarifa ya mchezo wa bao kuingizwa kwenye orodha ya michezo itakayoshindaniwa duniani kama ilivyo mingine.

Taarifa iliyotolewa jana na Shirikisho la Mchezo wa Bao Tanzania (SHIMBATA), iliyosainiwa na Rais wake, Monday Likwepa, ilisema kuwa mbali na kiongozi huyo, viongozi waandamizi wa wizara na taasisi mbalimbali za umma na watu binafsi watahudhuria, pamoja na wanachama na wadau wa mchezo huo.

Hafla ya kupokea taarifa hiyo, inatarajiwa kufanyika kwenye Ukumbi wa Makumbusho ya Taifa Jijini Dar es Salaam, mkabala na Chuo Kikuu cha Usamamizi wa Fedha (IFM).

Taarifa hiyo ilisema kuwa mchezo huo ulipitishwa kwenye orodha ya michezo itakayoshindaniwa duniani, kupitia shindani la tano la Utamaduni Duniani lililoandaliwa na World Nomad Games kwa ushirikiano na Umoja wa Mataifa kupitia UNESCO lililofanyika Septemba 7 hadi 14, mwaka huu, nchini Qazakhstan.

"Tunayo furaha kujulisha kuwa tumefanikiwa kuuingiza mchezo huu katika orodha ya michezo itakayoshindaniwa duniani.

Tumetekeleza kwa vitendo azma na ndoto ya Mwasisi waTaifa, Hayati Julius Kambarage Nyerere ambaye alitamani kuona bao inakuwa ni miongoni mwa michezo mikubwa duniani, yeye mwenyewe akiwa mpenzi na mchezaji wa mchezo huo, akiwakaribisha na kuwafundisha marais mbalimbali duniani kucheza mchezo huo.



## ZISIKUPITE

### PULISIC ATAKIWA UNITED

KLABU ya Manchester United inavutiwa na winga wa AC Milan na Marekani, Christian Pulisic, 26, pamoja na Liverpool na West Ham. ***(Kalciomercato)***

### KELLEHER AWANIWA CHELSEA

CHELSEA inapanga kumnunua kipa wa Liverpool na Jamhuri ya Ireland, Caoimhin Kelleher, 25, msimu ujao wa majira ya kiangazi. ***(Sun)***

### AMORIM BAJETI NDOGO

RUBEN Amorim anatazamiwa kufanya kazi kwa bajeti ndogo zaidi kuliko ya kocha wa zamani wa Manchester United, Erik ten Hag na atakuwa na jukumu la kuongeza uwezo ambao haujatumiwa katika kikosi huku klabu hiyo ikilenga kumaliza mzunguko mbaya na wa gharama kubwa wa marekebisho makubwa. ***(Telegraph)***

### ERIKSEN KUONDOKA UNITED

KIUNGO wa kati wa Manchester United, na Denmark, Christian Eriksen, anapanga kuondoka katika klabu hiyo msimu huu na hakuna mazungumzo yanayoendelea kati ya pande hizo mbili kuhusu mkataba mpya. ***(Fabrizio Romano)***

### ZIRKZEE KUMPISHA OSIMHEN

MANCHESTER United pia wanatafuta makubaliano ya kubadilishana ambayo yatamfanya mshambuliaji wao wa Uholanzi, Joshua Zirkzee, 23, ajiunge na Napoli, huku mshambuliaji wa Nigeria, Victor Osimhen, 25, akielekea Old Trafford. ***(Kalcio Napoli)***

### MCATEE AIVUTIA FULHAM

KLABU ya West Ham na Fulham zote zinavutiwa na kiungo wa kati wa Manchester City na England, James McAtee, 22. ***(Guardian)***

### RAPHINHA ATAKIWA ARSENAL

ARSENAL inavutiwa na mshambuliaji wa Brazil, Raphinha, 27, na imeripotiwa kuandaa ofa inayokaribia pauni milioni 75. Hata hivyo, Barcelona hawako tayari kuachana na mchezaji huyo kwa chini ya pauni milioni 83. ***(Fichajes)***

### LIVER, ARSENAL KUKWAMA

LIVERPOOL na Arsenal haziataweza kumsajili winga wa Ghana, Mohammed Kudus, 24, mwenye thamani ya pauni milioni 85, msimu ujao, kwani West Ham wanapania kumbakiza mchezaji huyo. ***(Football Insider)***

### MURILLO HAENDI KOKOTE

KLABU ya Nottingham Forest itapuuza ofa zozote za kumtaka mlinzi wao raia wa Brazil, Murillo, 22, Januari huku Real Madrid ikiwa miongoni mwa klabu zinazomtaka. ***(Football Insider)***

### CHIESA KURUDI ITALIA

WINGA wa Liverpool, Federico Chiesa mwenye umri wa miaka 27, anaweza kurejea nchini kwao Itali Januari huku Inter Milan wakitarajia kumsajili kwa mkopo. ***(Mirror)***

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# WAKALA AKATAA WAZO NEYMAR KURUDI SANTOS

**RIYADH,** Saudi Arabia

WAKALA wa Neymar, Pini Zahavi, amejibu uvumi unaodai kwamba mteja wake amekubali kuondoka Al Hilal na kurejea katika klabu yake ya utotoni ya Santos.

**Mshambuliaji huyo wa zamani wa Barcelona alirejea kutoka kwenye jeraha la mwaka mzima mwishoni mwa Oktoba, lakini ameumia tena.**

Neymar alirejea dimbani na kucheza kwa dakika 13 na hakuweza kumaliza mechi yake ya pili akitokea benchi, akichechemea kutokana na tatizo la misuli ya paja dhidi ya Esteghlal FC mapema Novemba hii kwenye Ligi ya Mabingwa Asia.

**●●● Yupo chini ya mkataba na ana furaha sana, sijui uvumi huu unatoka wapi...**

Kwa ujumla Neymar amecheza kwa chini ya dakika 500 katika kikosi cha kwanza cha Al Hilal kwa kipindi cha takriban miezi 18, na kusababisha uvumi kwamba mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 32, alikuwa anafikiria kuondoka Saudi Arabia.

Uhamisho wa kurejea Santos nchini Brazil uliripotiwa, lakini mwakilishi wa mchezaji huyo aliharakisha kufuta madai hayo na kuita ni ya uwongo.

"Hakuna mazungumzo yanayoendelea kwa Neymar kuondoka Al Hilal," alisema Zahavi akimwambia Fabrizio Romano.

"Yupo chini ya mkataba na ana furaha sana. Baba yake Neymar na mimi, sisi ndio watu pekee ambao tunaweza kuzungumzia mustakabali wa Ney. Sijui uvumi huu unatoka wapi."

Rais wa Santos, Marcelo Teixeira, alichochea uvumi mapema mwezi huu alipotoa mwaliko wa wazi kwa mchezaji huyo.

"Sisi tuko wazi na tuna lengo, baba yake na wafanyakazi wake wanajua," alisema.

# AMORIM AANZA RASMI KUINOA MAN UNITED




**MANCHESTER,** England

RUBEN Amorim ameongoza mazoezi yake ya kwanza kama kocha mkuu wa Manchester United baada ya kuidhinishwa kwa visa yake, kwa mujibu wa ESPN.

Amorim aliongoza mazoezi hayo huko Carrington siku ya Jumatatu kabla ya mechi yake ya kwanza dhidi ya Ipswich Town kwenye Uwanja wa Portman Road Jumapili. Wachezaji Marcus Rashford na Casemiro, wameripoti mapema baada ya kupewa likizo kutokana na ushindi wa mabao 3-0 dhidi ya Leicester City.

Kikosi kilichosalia kinatarajiwa kurejea kesho Jumatano au Alhamisi.

Wachezaji wanaopitia programu za utimamu ikiwa ni pamoja na Luke Shaw, Kobbie Mainoo, Mason Mount na Leny Yoro, walikutana na Amorim na wafanyakazi wake wiki iliyopita. Kwa mujibu wa chanzo hicho, kocha huyo mwenye umri wa miaka 39, na wasaidizi wake walipata vibali vyao vya kufanya kazi wiki iliyopita.

Amorim aliwasili Manchester wiki moja iliyopita na amekuwa akifanya mikutano huko Carrington. Alitembelewa Old Trafford Alhamisi kabla ya kufanya mahojiano yake ya kwanza kwenye kituo cha runinga cha ndani cha klabu hiyo, MUTV.

Kwa sasa anapanga kufanya mkutano wake wa kwanza na wanahabari Alhamisi au Ijumaa kabla ya kikosi hicho kusafiri hadi Ipswich Jumamosi. Amorim anakabiliwa na ratiba yenye shughuli nyingi kuanza utawala wake kwa michezo tisa ndani ya mwezi mmoja kabla ya Krismasi.

"Wakati Manchester United walipozungumza nami, waliniambia kuhusu mipango yao na unasisimka," alisema Amorim akiiambia MUTV.

# Pogba hana mpango kucheza nje ya Ulaya

**MIAMI,** Marekani

PAUL Pogba amedhamiria kuendelea na soka lake katika mojawapo ya ligi tano bora barani Ulaya baada ya kuvunjwa kwa mkataba wake na Juventus wiki iliyopita, vyanzo viameimbia ESPN.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 31, anaweza kurejea mazoezini Januari mwakani kabla ya kumaliza kifungo chake alichofungiwa kutokana na matumizi ya dawa zilizopigwa marufuku Machi.

Vyanzo viliiambia ESPN kwamba Pogba anaependelea kucheza katika moja ya ligi tano Ulaya ili kupata nafasi nzuri ya kurudisha nafasi yake katika kikosi cha Ufaransa kinachonolewa na Didier Deschamps.

Vyanzo hivyo viliongeza kuwa klabu kadhaa zimekuwa zikiwasiliana na wawakilishi wa wachezaji juu ya uwezekano wa kumsajili, ingawa hakuna mazungumzo kamili. Kwa sasa Pogba anafanya mazoezi huko Miami nchini Marekani ili kujiweka fiti.

Alipoulizwa na ESPN mwezi uliopita kuhusu wapi atacheza, mshindi huyo wa Kombe la Dunia alisema: "Lengo langu kuu kwa sasa ni kujiweka tayari. Ninaendelea na mazoezi ili nijitayarishe kwa ajili ya kujiunga na timu Januari."

Pogba hajacheza tangu Septemba 3, 2023, na alikuwa mchezaji ghali zaidi katika historia alipojiunga na Manchester United kutoka Juventus kwa ada ya euro milioni 105 mwaka 2016.

Pogba aling'ara katika ushindi wa Kombe la Dunia la Ufaransa mwaka 2018 na akarejea Juventus kama mchezaji huru mwaka 2022, lakini majeraha yalimfanya kucheza mechi nane pekee za Serie A katika kipindi chake cha pili katika klabu hiyo.



# *Pochettino akunwa na kiwango Marekani*



**ST. LOUIS,** Marekani

KOCHA wa Timu ya Taifa ya Marekani, Mauricio Pochettino, amesema "nilivutiwa sana" kuona wachezaji wake wakifanya vema katika ushindi wa mabao 4-2 wa dhidi ya Jamaica katika robo fainali ya Ligi ya Mataifa ya Concacaf.

Marekani walikuwa mbele kwa mabao 3-0 hadi mapumziko kwa mabao mawili ya Christian Pulisic na lingine kutoka kwa Ricardo Pepi.

Jamaica walijibu mapigo katika kipindi cha pili kwa mabao mawili ya Demarai Gray, lakini Tim Weah akafunga la nne na kuwaacha hoi 'Rege Boyz' hao.

Na hili lilifanya Pochettino - ambaye amekuwa kazini kwa miezi miwili - akifurahishwa na jinsi timu ya Marekani ilivyoonesha kiwangoa bora.

"Nimefurahishwa sana. Dakika 45 za kwanza ni jinsi tunavyotaka kukua, kujenga safari yetu pamoja na nadhani ilikuwa ya kustaajabisha kuona mchezaji akifanya vizuri," alisema.

"Katika kipindi kifupi, nadhani kwa jinsi wanavyobadilika na kupokea dhana zote na kwa jinsi tunavyojaribu kucheza, nadhani wanaonesha kuwa tuna wachezaji wazuri na wenye uwezo wa kuelewa na kujifunza haraka."

Pochettino alibainisha kuwa hakufurahishwa na jinsi kipindi cha pili kilivyokuwa, huku Rege Boyz wakifunga mara mbili.

Alisema kuwa kikosi chake kilihitaji kutafuta njia ya kubadili mfumo kabla ya kufungwa bao.

## HABARI MICHEZO

## Ramovic aanza kwa mkwara

INATOKA UK. 24

nyuma kwenye viwanja hivyo ili nijifunze mengi na vitu vipya," alisema kocha huyo.

Kocha huyo alitangazwa mwishoni mwa wiki kuchukua nafasi ya Miguel Gamondi raia wa Argentina ambaye aliondolewa kwenye kikosi hicho kwa sababu ambazo hazijawekwa wazi na uongozi, lakini wengi wakihusisha na vipigo viwili mfululizo ilivyovipata dhidi ya Azam FC kwa bao 1-0 na Tabora United mabao 3-1.

Klabu hiyo pia ilimtanga Kodro kutwaa nafasi ya aliyekuwa Kocha Msaidizi, Moussa N'Daw, raia wa Senegal, aliyetimuliwa pamoja na bosi wake.

Aidha, Yanga imemtangaza, Abdulhamid Moallin, aliyekuwa Kocha Mkuu wa KMC, kuwa Mkurugenzi wa Ufundi wa klabu hiyo.

## Msuva aipeleka Stars AFCON

INATOKA UK. 24

Watanzania kuona Taifa Stars ikifuzu AFCON kwa mara ya nne.

Baada ya kumalizika kwa mchezo huo, Msuva ambaye hilo ni bao lake la 24 kuifungia Stars tangu aanze kuichezea, alisema analitoa zawadi bao hilo kuwafariji waathirika wote wa ajali ya kuanguka kwa ghorofa Kariakoo, lakini pia akimshukuru Rais wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan kwa kuwaunga mkono na kuwafanya mashabiki kuujaza uwanja kuwasapoti.

"Tulipanga kupambana na tumepambana mpaka mwisho, tunashukuru kupata bao hili," alisema Msuva ambaye ni mfungaji namba mbili wa wakati wote Taifa Stars, akiwa nyuma ya Mrisho Ngassa mwenye mabao 25, huku wa tatu akiwa ni Mbwana Samatta na mabao yake 22.

Kocha Hemed Suleiman 'Morocco', alisema: "Haikuwa kazi nyepesi, wachezaji walipambana sana, nashukuru tumefanikiwa".

# FADLU: HATUTAIDHARAU PAMBA JIJI FC LIGI KUU

**Na Adam Fungamwangwo**

KOCHA Mkuu wa Simba, Fadlu Davids, amesema hawatoidharau Pamba Jiji kwa sababu tu haifanyi vema kwenye mechi zake za Ligi Kuu, badala yake wamejindaa vizuri na kuweka nguvu kubwa katika mchezo huo utakaochezwa, Uwanja wa CCM Kirumba, Mwanza, Ijumaa ijayo.

Akizungumza juzi jijini Dar es Salaam, kocha huyo raia wa Afrika Kusini, alisema waliiomba mechi hiyo kwa makusudi kwa ajili ya kuwapa mazoezi, utimamu wa mwili na uchangamfu wachezaji wake kabla ya kuivaa Bravo do Maquis ya Angola katika mchezo wa raundi ya kwanza, Kombe la Shirikisho Afrika hatua ya makundi utakaopigwa, Uwanja wa Benjamin Mkapa, Novemba 27, mwaka huu.

**Alisema kwa sababu waliuomba, basi watafanyia kazi kwa jinsi walivyouhitaji, yaani uwe wa maandalizi na pia kuhitaji pointi tatu za kuzidi kukaa juu kileleni mwa msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara.**

"Ni mchezo muhimu sana kwetu, tuliuhitaji na tunautaka tuucheze kwa nguvu kama vile tunacheza mechi ya kimataifa, kwa sababu tunajiandaa na hilo, kwa kutambua hilo, nilitaka mechi ya kirafiki kwa ajili ya mechi ya Pamba Jiji," alisema Fadlu.

Simba ilicheza mechi yake ya kirafiki mwishoni mwa wiki dhidi ya KMC kwenye Uwanja wa KMC Complex, Mwenge, Dar es Salaam, ambapo kwa mujibu wa Fadlu ulikuwa ni wa kujiandaa dhidi ya Pamba Jiji, huku wa Pamba ni wa kujiandaa dhidi ya Bravo do Maquis.

Awali mchezo huo uliahirishwa na Bodi ya Ligi, lakini uongozi wa Simba uliomba urudishwe ambapo taarifa zinasema Fadlu mwenyewe ndiye aliyeomba.

Kocha huyo pia alitoa siri ya kuichagua KMC na si timu nyingine, akisema anavutiwa na aina yao ya soka ambayo aliona inamfaa kwa ajili ya kuwatengeneza vijana wake.

"Katika timu zote alizoziona Tanzania, wao ndiyo wanacheza soka safi ambalo kama ukicheza nao kuna kitu unakipata kwenye masuala ya ufundi na ilikuwa hivyo, tulipata kipimo sahihi kweli," alisema.

Kikosi cha Simba kinatarajiwa kuondoka Alhamisi kwenda Mwanza kwa ajili ya mchezo huo, ikiwa kileleni mwa msimamo wa Ligi Kuu kwa pointi 25, ikicheza michezo 10.

Pamba Jiji ambayo itakuwa nyumbani ipo nafasi ya 15 ya msimamo wa Ligi Kuu, ikiwa na pointi nane kwa michezo 11, baada ya kushinda mchezo mmoja tu mpaka sasa, sare tano na kupoteza mitano, lakini pia ikiwa haijashinda mchezo wowote ikicheza uwanja wake wa nyumbani, CCM Kirumba.

**WANGU HUU...**



Mshambuliaji wa Taifa Stars, Clement Mzize, akimiliki mpira dhidi ya beki wa Guinea, Ibrahim Diakite, kwenye mechi ya Kundi H kuwania kufuzu Fainali za Mataifa ya Africa (AFCON) 2025, iliyopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam jana na kumalizika kwa wenyeji kushinda bao 1-0, lililoiwezesha kukata tiketi ya kushiriki michuano hiyo hapo mwakani nchini Morocco. **NA MPIGAPICHA WETU**

# Tabora United yapania mauaji kwa Singida Big Stars

**Na Mwandishi Wetu**

BAADA ya kufanya sherehe ya wiki nzima kwa kuifunga Yanga mabao 3-1 Novemba 7, mwaka huu, sasa kikosi cha Tabora United kimeanza rasmi mazoezi kujiandaa na mchezo ujao dhidi ya Singida Black Stars huku kikitamba kuwa timu hiyo itakipata kile ambacho kiliwakuta wenzao katika mechi hiyo itakayopigwa Uwanja wa Ali Hassan Mwinyi Jumapili ijayo.

Ofisa Habari wa klabu hiyo, Christina Mwagala, amesema wachezaji wote wa timu hiyo walianza mazoezi juzi, isipokuwa Salum Chuku ambaye ni majeruhi na wamekuwa na ari na nguvu kubwa baada ya kuonekana kuwa mashujaa kwa kuifunga Yanga.

"Baada ya kupata heshima kubwa na zawadi kutoka kwa watu mbalimbali na mashabiki wa soka nchini, wachezaji wa Tabora United wameanza mazoezi kwa ari na nguvu kubwa, tunachohitaji kwa sasa ni kuendeleza mlolongo wa ushindi, hatukuanza vizuri ligi, lakini tumeshinda mechi tatu mfululizo, tunataka tuendeleze ushindi na lengo letu mwisho wa msimu tuwe ndani ya zile timu nne za juu, ndiyo tunalohitaji msimu huu," alisema Mwagala.

Aliitahadharisha Singida Black Stars kuwa kama wakija vibaya, basi kile ambacho kiliwakuta Yanga nao kitawakuta na huenda idadi ya mabao ikawa kubwa zaidi.

"Hapa tunaandaa dozi kwa Singida Black Stars, tunawaambia wakija ovyo, watakutana na alichokutana nacho Yanga, na yeye vile vile kitakwenda kumkuta, kwa sababu mchezo huu unachezwa nyumbani na mashabiki wetu wengi watahudhuria kwani wamehamasika sana baada ya ushindi dhidi ya Yanga, kutokana na hilo hatutaki kuwapa tena huzuni na kuwapoteza mashabiki wetu," alisema Ofisa Habari huyo.

Baada ya kutofanya vizuri kwenye michezo kadhaa ya Ligi Kuu kiasi cha kumfukuza kocha wake, Francis Kimanzi, hasa baada ya kuchapwa mabao 4-2 dhidi ya JKT Tanzania, Oktoba 18, mwaka huu, timu hiyo ilishinda mechi tatu mfululizo, ikifunga Pamba Jiji bao 1-0, Mashujaa FC 1-0, kabla ya kuitwanga Yanga mabao 3-1.

Ipo nafasi ya sita kwenye msimamo wa Ligi Kuu, ikiwa na pointi 17, ikicheza mechi 11, ikishinda tano, sare mbili na kupoteza nne.

# Michezo

Jumatano Novemba 20, 2024

Nipashe




Wakala akataa Neymar kurudi Santos UKURASA 21

# MSUVA AIPELEKA STARS AFCON 2025

**Adam Fungamwango na Faustine Shija**

## ●●● Apiga bao la 24 akibakiza moja kumfikia Ngassa, Tanzania yafuzu mara ya nne, Mzize amgomea kocha...

BAO la dakika ya 60 lililofungwa na winga wa kimataifa, Simon Msuva, anayecheza soka la kulipwa Klabu ya Al Talaba ya Iraq, limeipeleka Tanzania fainali za Mataifa ya Afrika zitakazofanyika mwakani nchini Morocco.

Katika mchezo huo wa raundi ya sita hatua ya makundi, uliochezwa jana Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam, dhidi ya Guinea, Msuva alipachika bao kwa kichwa na kuifanya Taifa Stars kutoka na ushindi wa bao 1-0, katika mchezo huo wa Kundi H.

Lilionekana shambulizi lisilo na madhara lililotengenezwa taratibu ukiguswa na wachezaji kadhaa wa Stars mpaka ndani eneo la hatari, ukamkuta Mudathir Yahaya akaunyanyua mpira juu na Msuva kuuzamisha mpira kimyani kwa kichwa.

Beki wa kati wa Guinea, Ibrahima Conte, alijitahidi kuruka juu kutaka kuokoa, lakini ulimzidi kimo, mbele ukatua kidogo usawa wa kichwa cha Msuva ambaye hakufanya ajizi, akajitwisha na mpira ukajaa wavuni, licha ya jitihada za kipa Moussa Camara anayeichezea Klabu ya Simba kutaka kuokoa.

**Bao hilo liliamsha shangwe, hoihoi na nderemo kwa mashabiki wa soka waliokuwa uwanjani ambao walijazana kwa wingi kuangalia mchezo huo na kuipa nguvu Stars.**

Ushindi huo unaifanya Stars kufuzu fainali hizo ikimaliza kwenye nafasi ya pili nyuma ya Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo, ikikusanya pointi 10, mabao matano, ikifungwa nanne, ikishinda michezo mitatu, sare moja na kupoteza miwili.

DR Congo imeshafuzu ikiwa na pointi 12, jana ikitarajia kucheza mchezo wake wa mwisho wa kumalizia dhidi ya Ethiopia.

Kipigo hicho kimeifanya Guinea kumaliza michezo sita ikiwa na pointi tisa, ikishika nafasi ya tatu kwenye kundi hilo.

Timu mbili zitakazomaliza nafasi za juu katika makundi yote 12, yaliyopangwa na Shirikisho la Mpira wa Miguu Afrika (CAF), zitafuzu fainali hizo, huku nyingine zikiwa tayari zimeshafuzu.

Hii ni mara ya nne kwa Stars kufuzu fainali hizo, mara ya kwanza ikiwa ni 1979, ambapo fainali zake zilipigwa nchini Nigeria mwaka 1980, mara ya pili ikiwa ni 2019, ambapo fainali zake zilichezwa nchini Misri na ya tatu ilikuwa 2023 ambapo fainali zake zilichezwa mwaka huu nchini Ivory Coast.

Katika mchezo huo wa jana, dakika ya kwanza tu, tayari Stars ilikuwa imeshafika langoni mwa Guinea kwa shambulizi lililofanywa na nahodha Mbwana Samatta, lakini kipa Camara akikaa imara la kuzima jaribio hilo.

Guinea ilijibu kwa shambulio hilo dakika moja baadaye kupitia kwa Sylla Morlaye, lakini mabeki wa Stars wakiongozwa na Ibrahim Hamad 'Bacca' walikaa imara na kuokoa hatari.

Dakika ya nne, Stars ilirejea tena langoni mwa wageni wao, safari hii, Samatta alimpa pasi ya kurudisha Mudathir, nje kidogo ya eneo la hatari, alipiga shuti kali ambalo liliwababatiza mabeki wa Guinea na kuwa kona tasa.

Krosi ya Clement Mzize ilikosa muunganishaji dakika ya sita, na dakika ya 10, Msuva alikosa bao la wazi akiwa ameliangalia lango huku mashabiki na watu wa benchi la ufundi wakiwa tayari wamesimama kushangilia.

Ilikuwa ni krosi safi kutoka kwa Shomari Kapombe, iliyomkuta akiwa kwenye nafasi nzuri kabisa, lakini shuti lake lilikwenda pembeni kwa mshangao wa wengi akiwa hatua sita tu kutoka langoni.

Camara alilazimika kufanya kazi ya ziada dakika ya 15, kwa kuokoa krosi ya Kapombe iliyokuwa inakwenda kutua kwenye kichwa cha Samatta.

Mzize itabidi ajilaumu mwenyewe kwa kukosa mabao mawili ya wazi, dakika ya 27 na 33, huku baadaye akionekana kuumia na benchi la ufundi lilitaka kumtoa nafasi yake ichukuliwe na Kibu Denis, lakini alikataa kutoka. Pamoja na kukataa kutoka nje, alikosa tena bao la wazi dakika 40.

Hata hivyo, hakurejea tena kipindi cha pili nafasi yake ikachukuliwa na Kibu ambaye kwa kiasi kikubwa aliongeza uhai akisaidia ulinzi na kuanzisha mashambulizi mengi hadi ilipofika dakika iliyokuwa inasubiriwa na mamilioni ya

INAENDELEA UKURASA 23



Mshambuliaji wa Taifa Stars, Mbwana Samatta, akimbeba mfungaji wa bao pekee, Simon Msuva, aliyeipeleka Tanzania Fainali za Mataifa ya Africa (AFCON) 2025, baada ya kuibuka na ushindi wa bao 1-0 dhidi ya Guinea kwenye mechi ya Kundi H ya kuwania kufuzu fainali hizo iliyopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam jana. **NA MPIGAPICHA WETU**

## Ramovic aanza kwa mkwara mzito Yanga

**Na Adam Fungamwango**

HATIMAYE Kocha Mkuu mpya wa Yanga, Sead Ramovic, raia wa Ujerumani ameanza kukinoa kikosi hicho kwa kishindo na mkwara mzito, kuelekea kwenye mchezo wa raundi ya kwanza, Ligi ya Mabingwa Afrika, hatua ya makundi dhidi ya Al Hilal Omrudman ya Sudan, utakaopigwa, Novemba 26, mwaka huu, kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Kwanza kabisa kocha huyo aliingia kwa mara ya kwanza juzi kwenye Uwanja wa Avic Town uliopo Kigamboni, Dar es Salaam na kuanza kuukagua kabla ya kufanya kitu chochote kile, akiwa ameongozana na kocha wake msaidizi mpya, Mustapha Kodro, raia wa Bosnia & Herzegovina.

Aliingia na kutembea akizunguka maeneo ya uwanja na kuna wakati alikuwa akiinama chini na mkono wake ulikuwa unakagua ubora wa nyasi na udongo ndani ya uwanja huo.

Baadaye alionekana kunong'ona kitu na msaidizi wake na baadaye walikwenda kuungana na benchi zima la ufundi, akiwamo meneja wa timu hiyo, Walter Harrison, ambaye alionekana kupiga stori kwa muda mrefu na kocha huyo mpya.

Mazungumzo yalipomalizika, walipeana mikono watu wote wa benchi la ufundi na waliingia uwanjani pamoja na wachezaji mazoezi yakaanza.

Mazoezi ya mwanzo yalionekana kuwa ya kurudisha utimamu wa mwili uliopotea baada ya mapumziko, huku kwa vipindi fulani wachezaji wakichezea mipira.

Kocha huyo alisema anatamani kufanya kazi saa 24 ili kuhakikisha anaiimarisha timu hiyo kwani ina wachezaji bora.

"Nina imani bado nina vitu vingi vya kuwaongezea kimbinu na kiufundi, nadhani changamoto kubwa itakuwa ni kujifunza hukusu ligi hii, nimepewa taarifa kuwa kuna baadhi ya viwanja si vizuri eneo la kuchezea, inabidi ubadili mbinu ili uweze kupata matokeo mazuri, hivyo naendelea kutazama mechi ilizocheza Yanga huko

INAENDELEA UKURASA 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >